

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Tisa – Tarehe 14 Septemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali yetu Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti maalum sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Na.109

Serikali Kufuta Sherehe za Mwenge

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MHE. ZUBEDA H. SAKURU) aliuliza:-

Sherehe za Mwenge wa Uhuru zimeendelea kutumia fedha nyingi za walipa kodi huku Watanzania wengi wakiwa na maisha duni. Je, Serikali haioni umuhimu wa kurudisha Mwenge wa Uhuru katika Makumbusho ya Taifa na kuzifuta sherehe hizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, AJIRA NA VIJANA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeda Hassan Sakuru, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenge wa Uhuru ni chombo kilichoasisiwa na Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mwaka 1961 ikiwa ni tunu na ishara ya kuwepo kwa Taifa huru la Tanganyika. Dhana na falsafa ya Mwenge wa uhuru inatokana na maono ya mbali kupitia kwenye maneno yaliyosemwa tarehe 9 Desemba, 1961 nanukuu:-

"Sisi tumekwisha uwasha Mwenge wa Uhuru na kuuweka juu ya Mlima Kilimanjaro umulike ndani na nje ya mipaka yetu, ulete matumaini pale ambapo hakuna matumaini, ulete upendo mahali penye chuki na heshima mahali palipojaa dharaau"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni umuhimu wa kuweka Mwenge wa Uhuru katika makumbusho ya Taifa na kuzifuta sherehe zake kwa sababu zifuatazo:-

(i) Mbio za Mwenge wa Uhuru huwakumbusha Watanzania falsafa nzito ya Mwenge wa Uhuru inayotoa taswira ya Taifa ambalo Waasisi wetu walitaka kulijenga Taifa lenye amani, linalojitegemea na lenye kuheshimu misingi ya utu na usawa wa binadamu. (*Makof!*)

(ii) Mwenge wa Uhuru kupitia mbio zake umekuwa ni chombo cha kuchochaea maendeleo ya wananchi, kwa mfano, kwa kipindi cha miaka mitano iliopita, miradi ya maendeleo 6,921 yenye thamani ya shilingi triliioni 2.5 ilizinduliwa na kuwekewa mawe ya msingi. (*Makof!*)

(iii) Kila mwaka, Mbio za Mwenge huambatana na ujumbe maalum unaohamasisha masuala muhimu ya Kitifa kwa wananchi nchi nzima. Kwa mfano, kwa mwaka jana 2017 ujumbe ulikuwa "Shiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya nchi yetu". Mwaka huu wa 2018 ujumbe ni "Elimu ni ufunguo wa maisha, wekeza sasa kwa maendeleo ya Taifa letu". Aidha, kila mwaka wananchi hukumbushwa kuendelea na mapambano dhidi ya UKIMWI, malaria, rushwa na dawa za kulevya. (*Makofi*)

(iv) Mwenge wa Uhuru unaimarisha Muungano wetu, Mwenge wa Uhuru huzunguka nchi nzima Tanzania Bara na Zanzibar. Wanaokimbiza Mwenge wa Uhuru wanatoka sehemu mbili za Muungano. Kwa kufanya hivyo, Mwenge wa Uhuru unazidi kutuunganisha kama watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si kweli kwamba Mwenge wa Uhuru unatumia fedha nyingi za walipa kodi. Kwa mfano, kwa mwaka 2017, Serikali ilitenga shilingi milioni 463 kugharamia shughuli za Mwenge wa Uhuru ukilunganisha na kiasi cha miradi 1,582 iliyozinduliwa yenye thamani ya shilingi trilioni 1.1 ni dhahiri kuwa hoja ya gharama kuwa kubwa siyo ya msingi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Majibu ya swali yamejitoshelleza hatuwezi kuchukua tunu ya Taifa tukaipeleka kwenye makumbusho. Tunaendelea na swali lingine, Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijaauliza maswali ya nyongeza.

WABUNGE FULANI: Hajauliza maswali ya nyongeza.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge
Waliongea bila mpangilio)*

MWENYEKITI: Majibu ya swali yamejitoshelleza Mheshimiwa Sophia.

WABUNGE FULANI: Aaaaaaa.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge Waliongea bila mpangilio)*

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Haiwezekani, hicho kitu hakipo.

MWENYEKITI: Tuendelee na Mheshimiwa Haji Dau.

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge Waliongea bila mpangilio)*

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kinyume na Kanuni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dau.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Swali la nyongeza sijaauliza.

MBUNGE FULANI: Limejitosheleza nini, Kanuni gani mnayofuata?

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge Waliongea bila mpangilio)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba mtulie.

WABUNGE FULANI: Hatukubali, haijawahi kutokea.

MWENYEKITI: Nasema hivi majibu yamejitosheleza.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: *Why?*

MWENYEKITI: Hii ni tunu ya Taifa.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: *Why?* Sijaauliza swali la nyongeza, *why?*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa
Wabunge Waliongea bila mpangilio)*

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee. Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji swali lingine.

Na.110

Ucheleweshwaji wa Mishahara kwa Watumishi wa Umma

MHE. MWANTUMU DAU HAJI aliuliza:-

Kumekuwa na ucheleweshaji wa mishahara kwa watumishi wa umma:-

Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Waraka wa Hazina Na.12 wa mwaka 2004, watumishi wa umma wanatakiwa kulipwa mishahara yao kabla ya tarehe 25 ya kila mwezi. Kumbukumbu za malipo ya mishahara kwa watumishi wa umma zinaonyesha kuwa, kuanzia Julai, 2017 hadi Agosti, 2018 watumishi walilipwa mishahara yao kati ya tarehe 20 na 24 ya kila mwezi. Hivyo basi, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na umma kwa ujumla kuwa hakuna ucheleweshaji wa malipo ya mishahara kwa watumishi wa umma.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mantumu swali la nyongeza.

MHE. MWANTUMU DAU HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa hivi sasa. Kwa kuwa hakuna ucheleweshwaji wa mishahara, napenda kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Serikali inasema nini kuhusu uongezaji wa mishahara kwa watumishi hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali inasema nini kuhusu upandishaji wa madaraja mbalimbali kwa watumishi wa umma?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ameuliza Serikali inasema nini kuhusu uwekezaji wa mishahara ya wafanyakazi. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mshahara ni mali halali ya mfanyakazi mwenyewe hivyo kuhusu uwekezaji ni mfanyakazi mwenyewe anaamua mshahara wake nini aufanyie, akitaka kuuwekeza wote yuko huru kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu upandishwaji wa madaraja, Serikali yetu siku zote imekuwa ikiwatendea haki wafanyakazi wetu kwenye upandishaji wa madaraja na kila mwaka wafanyakazi hupandishwa madaraja.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Asha Abdallah Juma kwa niaba.

Na.111

VETA Kuingizwa Katika Sera ya Elimu ya Msingi

MHE. ASHA ABDALLAH JUMA (K.n.y. MHE. KHADIJA NASSIR ALI) aliuliza:-

Sera yetu ya Elimu inatueleza kuwa elimu ya msingi ni hadi kidato cha nne:-

Je, ni lini Serikali itaboresha kiwango hiki cha elimu ya msingi hadi kufika ngazi ya Ufundsi Stadi yaani **VETA**?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibuu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa elimu wa Tanzania unasihamiwa na Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Sheria hii inabainisha wazi kuwa elimu ya msingi ni miaka saba kuanzia Darasa la Kwanza hadi Darasa la Saba. Hivyo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, elimu ya msingi inatolewa kwa muda wa miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa elimu ya msingi kwa miaka saba bila kuunganisha na mafunzo ya ufundsi stadi. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni kwamba maudhui yaliyopo kwenye mtaala wa elimu ya msingi bado yanakidhi mahitaji ya sasa ya wahitimu wa ngazi hiyo ya elimu ya msingi lakini pia muda ambao wanafunzi wa elimu ya msingi wanakaa shulenii hauwezi kutosha kuunganisha na mafunzo ya ufundsi stadi. Hivyo, mafunzo ya ufundsi stadi yataendelea kutolewa na Mamlaka ya Ufundsi Stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaendelea na jitihada za kuongeza nafasi za udahili katika Vyuo vya Mafunzo ya Ufundisti. Juhudi hizi ni pamoja na kujenga Vyuo vipyta vya Ufundisti na vilevile kufanya ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili viwe na mazingira fanisi ya kujifunzia na viweze kutoa mafunzo katika fani mablimbali.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Abdallah Juma.

MHE. ASHA ABDALLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, bado vijana wengi wanaomaliza darasa la saba wanakuwa hawajapata nafasi kwenye vyuo vya ufundisti au kuendelea na masomo ya sekondari. Ni lini Serikali itaboresha elimu ya msingi kuhusisha mafunzo ya ufundisti ndani yake ili kuwaasaidia wale wanaobaki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mtaala wa VETA ni mmoja nchi nzima wakati mahitaji yanatofautiana sehemu na sehemu. Kwa mfano, mikoa yenye gesi wangefundishwa mambo yanayotokana na gesi, mikoa ya uvuvi wangefundishwa taaluma za uvuvi na mikoa ya madini vivyo hivyo. Sasa Serikali ina utaratibu gani kuhusu kuingiza *component* hiyo katika mitaala yake?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuhusu suala la wanafunzi ambao wanamaliza darasa la saba lakini hawapati nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari, kama ambavyo nimesema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali inafanya kazi kubwa ya kuongeza nafasi za udahili

kwenye vyuo vya ufundi kwa kujenga vyuo vipyta vya ufundi pamoja na kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niseme kwamba katika mtaala wa elimu ya msingi kuna somo la stadi za kazi ambalo limewekwa mahsus kwa ajili ya kuwapatia vijana wetu angalau ujuzi ili hata yule anayemaliza elimu yake ya msingi awe tayari ana uwezo wa kufanya jambo katika mazingira yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu mtaala wa *VETA* kwamba unafanana, kimsingi masuala ya ufundi yanatakiwa yaangalie mazingira halisi ya mahali ufundi unapofanyika. Kwa hiyo, suala la kuangalia masuala ya gesi au masuala ya uvuvi ndiyo jambo ambalo limekuwa likifanyika. Kwa hiyo, niendelee kutoa wito kwa wote wanaotoa mafunzo ya ufundi stadi wahakikishe kwamba mitaala yao inazingatia mazingira halisi ya pale ambapo wanatoa mafunzo ili kuwawezesha wananchi wa eneo husika kuongeza tija katika shughuli wanazozifanya.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwalongo nimekuona na Mheshimiwa Toufiq.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa sasa wa kutumia *VETA* na vyuo vya *FDC* kutoa mafunzo ya ufundi stadi umekuwa ni wa polepole sana na idadi kubwa ya vijana wanamaliza shule za sekondari hawana ujuzi kabisa. Je, Serikali inaonaje sasa ikaanza kubadilisha baadhi ya shule za sekondari ambazo tumezijenga katika Halmashauri zetu kuwa shule za ufundi ili kusudi zisaidie vijana hawa kupata elimu ya ufundi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwalongo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba Serikali tayari imeshaona hiyo changamoto na ndiyo maana zile shule za ufundi ambazo awali zilikuwa zimebadilishwa mafunzo ya ufundi yaliondolewa tayari Serikali imeshachukua jukumu la kuzikarabati zile shule saba za ufundi za Kitaifa na kuziimarishia vifaa vya kufundishia na karakana zake zote zimeimarishwa. Nitoe wito kama alivyosema Mheshimiwa Mwalongo, Serikali itafurahi sana kama kuna Halmashauri ambayo ina shule na wanaona kwamba inakidhi vile vigezo vya kutoa mafunzo ya ufundi tuko tayari watuambie ili twende kuikagua na tutapenda tu kuongezea idadi ya wanaofanya mafunzo ya ufundi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Toufiq.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa baadhi ya shule za msingi zina vituo vya ufundi stadi, mfano, katika Wilaya ya Chamwino, vituo hivyo viko katika Shule ya Msingi Mvumi Mission na Shule ya Msingi Chamwino lakini hakuna vifaa wala walimu wa kutosha. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvifufua vituo hivyo siyo kwa Wilaya ya Chamwino tu lakini katika shule zote za msingi ambazo ziko Tanzania hii? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLIJIA:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la dada yangu Mheshimiwa Fatma Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwa swali lake zuri kwa sababu ni kweli zile shule zipo lakini kwa kweli hali yake hajakaa vizuri, niliona nilipozitembelea. Kwa

hiyo, tayari Serikali imeliona na kwa kupitia Mradi wa Kukuza Ujuzi hapa Nchini (*ESPJ*) ambao Wizara yangu inautekeleza kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, tutafanya tathmini ya shule hizo na kwa awamu tutaanza kuzifanya maboresho kwa kuzipelekea vifaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Salma Kikwete.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunaamini na tunajua kwamba elimu ndio msingi wa kila kitu katika maisha ya mwanadamu na mafanikio ya elimu ni pamoja na kuwa na zana za kufundishia pamoja na kujifunzia. Kwa kuwa, vitabu vyetu vya kiada huchapishwa nje ya nchi yetu na tukiamini kwamba elimu ni jambo tete katika ustawi wa Taifa letu, je, ni lini vitabu hivi vya kiada vitachapishwa hapa nchini ukizingatia Serikali yetu ni ya viwanda? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru sana kwa kuleta swali hili hapa Bungeni na nitumie nafasi hii kuonyesha masikitiko yangu makubwa sana kwa makampuni ya Kitanzania ambayo yanafanya kazi ya uchapishaji. Haya Makampuni yametuangusha kweli kweli, tumelazimika kwenda kuchapa vitabu nje kwa sababu unapoyapa makampuni ya Kitanzania kwanza kuna mengine ambayo yamekuwa yanachapa vitabu, kitabu kimekaa kama sambusa yaani wanakata hovyo hovyo lakini pia wanatumia muda mrefu kuvichapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuhusu swali lake kwamba Serikali ina mpango gani, kutokana na changamoto hiyo, Serikali imeamua kununua mashine ya uchapaji na hapa tunapoongea tayari tumekwishiagiza.

Kwa hiyo, tunategemea hilo suala sasa tutakuwa tunalifanya wenyewe.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe aulize swali lake.

Na.112

Kufungua Mgodi wa Nyakafuru

MHE. AUGUSTINO M. MASELE aliuliza:-

Je, ni lini mgodi utafunguliwa katika eneo la Nyakafuru Wilayani Mbogwe baada ya utafiti kuchukua muda mrefu kwenye eneo hilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Nyakafuru lenye leseni ya ukubwa wa kilomita za mraba 17.53 linamilikiwa na Kampuni ya Mabangu *Limited Resources*, kampuni ambayo Kampuni tanzu ya *Resolute Tanzania Limited* kupitia leseni ya kutafuta madini PL Na.5374 ya mwaka 2008. Leseni hiyo ambayo ilihuishwa mara mbili na baadaye kuongezewa muda wa kipindi cha miaka miwili yaani *extension* kuanzia tarehe 24 Oktoba, 2016 ili kukamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na itamaliza muda wake tarehe 23 Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, marekebisho ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 yaliyofanyika mwaka 2017

yaani *The Written Laws Miscellaneous Amendment Act 2017* yaliondoa uhitaji wa leseni ya utafutaji wa madini kuongezewa muda wa kufanya utafiti baada ya muda wa leseni kuhuishwa kwa mara ya pili kumalizika. Kwa sasa sehemu ya eneo hilo la leseni hiyo imevamiwa na wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa mashapo yanayofikia takribani tani 3.36 yenye dhahabu ya wakia 203,000 yamegunduliwa na jumla ya Dola za Kimarekani milioni 1.83 zimetumika kufanya utafiti katika eneo la mradi. Aidha, Tathmini ya Athari ya Mazingira ilishafanyika na kupewa cheti cha tarehe 16/10/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, Kampuni ya Mabangu *Mining Limited* kuititia Kampuni mama ya *Resolute (Tanzania) Limited* inadaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kiasi cha jumla Sh.143,077,421,804 ikiwa ni deni la kodi ambalo wanatakiwa kulilipa. Mgodi wa Nyakafuru unaweza kuendelezwa baada ya deni hilo kuwa limelipwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masele.

MHE. AUGUSTINO M. MASELE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kwa kuwa eneo hili la Nyakafuru limekuwa chini ya utafiti kwa muda mrefu na tayari wachimbaji wadogo wameshalivamia. Je, Serikali iko tayari sasa kuwamilikisha wachimbaji hao wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, eneo pia la Nakanegere Mlimani nalo limekuwa chini ya utafiti kwa muda mrefu. Serikali inasemaje juu ya uwezekano wa kuwapatia wananchi kuchimba kwa leseni za wachimbaji wadogo wadogo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwamilikisha wananchi kwenye eneo hilo, nieleze tu kwamba Mheshimiwa Mbunge anafahamu wananchi wa Nyakafuru ndiyo wao wako pale wanaendelea na shughuli. Kwa kuwa wanaendelea na shughuli pale na kwa maelekezo tuliyopewa kazi yetu ni kuwasaidia wachimbaji wadogo, wale ambaو hawako rasmi tuwarasimishe ili waweze kupata vibali halisi waweze kuchimba kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la Nakanegere, eneo hili lote linamiliikiwa na kampuni moja na lenyewe utaratibu wake utakuwa kama ule wa Nyakafuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Umbulla, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Kama liliuyo suala la madini katika Jimbo la Mbogwe, Mkoa wetu wa Manyara maeneo mengi yana madini kulingana na utafiti uliofanyika. Hivi sasa uchimbaji huo unafanywa kiholela na sina hakika kama Serikali ina mkakati wowote ama ina taarifa na suala hilo. Je, Serikali sasa iko tayari kutupa takwimu ama hali halisi ya madini yaliyoko katika Mkoa wetu, Wilaya za Mbulu, Simanjiro na Kiteto?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO):
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bura atakumbuka kwamba wakati tunawasilisha bajeti yetu pamoja mambo mengine tulitoa machapisho na majarida mbalimbali ambayo ndani yake yalikuwa yanatoa takwimu kwa ujumla kwenye sekta ya madini kwa kila Mkao, Wilaya na maeneo mbalimbali. Naamini Mheshimiwa Bura akienda kukapitia kale kakijitabu atapata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili jambo lingine ambalo ameeleza juu ya wananchi kuchimba kwenye maeneo mbalimbali kwenye Mkao Manyara. Niseme kwamba Serikali inazo taarifa za wachimbaji wadogo kuvumbua. Mara ugunduzi unapotokea, kazi yetu ya kwanza ni kupeleka usimamizi ili kudhibiti usalama lakini vilevile kudhibiti mapato ya Serikali. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Bura ugunduzi wowote unaotokea katika Mkao wa Manyara tunafahamu na tayari kuna usimamizi ambao unafanywa na Ofisi zetu za Madini kwenye Kanda pamoja na Mikoa.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuweka taarifa sahihi, mimi naitwa Martha Umbulla na siyo Bura.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Martha Umbulla. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini sasa aulize swali lake.

Na. 133

**Vifo vyatya Askari wa Jeshi la Ulinzi
la Wananchi (JWTZ) Nje ya Nchi**

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED aliuliza:-

Kwa kipindi cha kirefu sasa nchi yetu imekuwa ikipeleka Askari wa Jeshi la Wananchi (JWTZ) nje ya nchi ambako kuna vita vya wenyewe kwa wenyewe na kusababisha misiba mikubwa sana kwa Askari wetu:-

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na kadhia hiyo?

MWENYEKITI: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGWA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kikanda kama *East Africa Community* na SADC na Jumuiya ya Nchi za Maziwa Makuu inao wajibu wa kushiriki katika Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali. Madhumuni ya kupeleka askari wetu huko ni kwenda kulinda amani na sio kushiriki kwenye mapigano. Kwa bahati mbaya sana, yapo matukio ya kushambuliwa kwa askari wetu yaliyofanywa na vikundi vya waasi yaliyopelekea kupoteza maisha ya baadhi ya askari wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limechukua hatua ya kutoa mafunzo ya kutosha kwa vikosi vyetu vinavyopewa jukumu hili, pamoja na kuwaongezea vifaa vya kisasa ili waweze kujilinda dhidi ya mashambulio ya vikundi vya waasi. Hivyo, mtazamo wa Serikali ni kuendelea kushiriki katika shughuli za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali ili kutimiza wajibu wetu Kimataifa na huku tukichukua kila tahadhari kuepusha maafa yaliyowahi kutokeea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Muhammed swali la nyongeza halafu Mheshimiwa Masoud.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Majibu ya Serikali hayatoshelezi, ni afadhal tu kidogo. Pamoja na majibu hayo, nina maswali mengine mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kuna kauli mitaani zinasemwa na Watanzania kwamba Tanzania inashiriki hasa hasa kwa maslahi binafsi ya kukomba mali za DRC kwa mfano. Je, Serikali ina matamshi gani kwa lengo la kuwaosha Watanzania kutokana na tuhuma hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Jeshi letu linapopigwa kwenye vita hasa pale *DRC* kuna kauli pia kwa Watanzania wanaamini kwamba Jeshi la Uganda linashiriki katika kulipiga Jeshi la Tanzania kwa kuwa wakati fulani kihistoria Waganda na Watanzania walipapurana kivita. Je, ni ipi kauli ya Serikali kuhusiana na kadhia hii? Ahsante.

MWENYEKITI: Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Muhammed Amour, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa bahati mbaya sana maneno kama haya yanatolewa na Watanzania ambao kwa kweli wanatakiwa wao wawe wazalendo na kuweza kupongeza juhudzi za Serikali za kuwasaidia wenzetu ambao wako katika hali ambayo haina amani katika nchi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna suala la kukomba mali za *DRC* kwa maslahi binafsi, halipo. Tanzania haishughuliki na kuchukua chochote sehemu yoyote wanayolinda amani. Majeshi yetu yako kule kusaidia kurudisha hali ya amani, kuwalinda wananchi dhidi ya waasi ambao wanapigana katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba Jeshi la Uganda linashiriki katika kuwapiga Watanzania pia halina ukweli wa aina yoyote. Matukio yote yaliyotokea tuna ushahidi wa kutosha kwamba ni vikundi vyta waasi. Mwanzoni walikuwa *M.23* na sasa hivi kuna vikundi vingine ambavyo

vinatokea katika nchi mbalimbali za jirani pale lakini hakuna ukweli kwamba Majeshi ya Uganda yanashiriki katika kuwapiga askari wa Tanzania. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nina swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna vikundi vya waasi ambavyo vinapelekea kufanya hujuma kwa Vikosi vyetu vya Kulinda Amani *DRC* - Kongo na maeneo mengine na pale inapotokea maafa kwa hawa askari wetu kupoteza maisha huwa kuna malipo maalum kutoka Umoja wa Mataifa lakini hata Serikali yetu nayo huwa kuna kiwango cha fedha ambacho wanatoa. Je, Serikali hasa ina mkakati gani wa ziada kuleta Muswada hapa Bungeni kuongeza muda wa kulipa wajane au wagane pale ambapo wanajeshi wanapoteza maisha katika kulinda amani *DRC* Kongo na Sudan Kusini na maeneo mengine? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Masoud, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Umoja wa Mataifa na Serikali ya Tanzania imekuwa ikilipa mafao yanayohusiana na ushiriki wa askari wetu katika Ulinzi wa Amani sehemu mbalimbali. Vinapotokea vifo basi kuna fedha maalum na kuna viwango maalum viliviyopangwa ambavyo hutolewa na Umoja wa Mataifa na Tanzania sisi tunatoa kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi na Kanuni za Majeshi zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuongeza fedha kwa wajane, ni suala ambalo tunalitafakari kwa madhumuni ya kuweza kuboresha maslahi yote kwa ujumla siyo moja moja. Kwa sababu kuna maslahi mengi ambayo wanajeshi hawa

wanatakiwa wayapate. Sasa hivi Sheria ya Ulinzi wa Taifa inapitiwa pamoja na Kanuni zake ili kuangalia ni viwango gani nya maslahi gani ambavyo vimepitwa na wakati ili viweze kuboreshwa kwa pamoja.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe Mbuge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 114

Mfumo Chakavu wa Mabomba ya Maji Nchini

MHE. LUCIA M. MLOWE aliuliza:-

Mfumo wa mabomba ya maji kwenye maeneo mengi nchini ni chakavu hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa maji:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kubadilisha mabomba yote chakavu katika nchi ili kuokoa maji yanayopotea kutokana na uchakavu huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucia Mlowe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sekta ya maji imekuwa inakabiliwa na changamoto ya upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu iliyojengwa miaka mingi iliyopita. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea na jitihada za uwekezaji katika ukarabati wa miundombinu chakavu maeneo mbalimbali ya mijini ikiwemo Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mwanza, Morogoro, Singida pamoja na ukarabati wa miradi ya kitaifa

ya Makonde, Wanging'ombe, Maswa, HTM, Mugango Kiabakari na Chalinze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Miradi ya Maji Vijijini, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeendelea kuimarisha Programu ya Uendelevu wa Huduma ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini kwa kutumia Mfumo wa Malipo ya kwa Matokeo (*Payment for Results -PforR na Payment by Results – PbR*) ambapo kwa pamoja zinalenga kuhakikisha kasi ya uendeshaji, matengenezo na ukarabati wa miundombinu ya miradi ya maji vijijini inakuwa endelevu na wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada hizo kwa pamoja zitasaidia kupunguza hali ya upotevu wa maji katika miradi ya maji mijini na vijijini.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mlowe, swali la nyongeza.

MHE. LUCIA M. MLOWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza, nina maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Waziri amekiri kwamba kuna tatizo la upotevu wa maji kutohana na miundombinu mibovu. Hivi navyoongea bado kuna tatizo kubwa sana la uvujaji wa maji, mfano, Kisasa kuna mabomba hivi sasa yanaendelea kutiririsha maji lakini sioni juhudhi inayoendelea hadi sasa hivi. Je, wana mkakati gani kuhakikisha tatizo hili linatatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Jimbo la Njombe Kusini, Kata ya Ihungilo kuna mradi wa Utengule – Ngalanga ambao vifaa vilivyonunuliwa vilinunuliwa chini ya kiwango na hadi sasa hivi vifaa hivi, mabomba na viungio vyake vinaendelea kutiririsha maji na wananchi wanakosa huduma ya maji. Je, Waziri yuko tayari kwenda kutatua tatizo hili katika Kata hii ya Ihungilo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mlowe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, upotevu wa maji ni changamoto kubwa kwa sababu lina sehemu mbili, kwanza ni miundombinu yenye na pili ni wafanyakazi tunasema *non commercial revenue water losses* ambalo linatokana na baadhi ya wafanyakazi kushirikiana na wananchi katika kuiba maji. Tunapamba na mambo yote haya mawili na kuhakikisha kwamba tatizo la upotevu wa maji linamalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema sasa hivi kuna changamoto hizo lazima mtu akiona changamoto hiyo tuwasiliane na Mamlaka za Maji, tuwape taarifa ili waweze kwenda kumaliza tatizo hilo. Kila kwenye Mamlaka ya Maji tumeweka *toll free number* ambayo ni namba ya simu ambapo unaweza kupiga simu bure kueleza wapi kuna tatizo la upotevu wa maji na mara moja utakapofanya hivyo sisi tutachukua hatua za kuweza kupambana na upotevu huo wa maji. Hili la Kisasa kama alivyosema Mheshimiwa naamini wataalam wangu wamesikia na watakwenda kulishughulikia mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu vifaa vilivyo chini ya kiwango. Ni kweli kabisa katika miradi mingi sana iliyojengwa vijijini, vifaa vingi vilivyopelekwa na wakandarasi viko chini ya kiwango na tumechukua hatua mbalimbali za kisheria na tutaendelea kuchukua. Naomba tu nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakwenda pamoja tuhakikishe kwamba tatizo hili tunaliondoa ili wananchi wale waweze kupata maji safi na salama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Willy Qambalo.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Miradi ya maji katika Vijiji vya Getamok, Endonyawed, Kansai, Mataala na Fusmai katika Wilaya ya Karatu ambayo ni zaidi ya asilimia 50 ya ile miradi kumi katika kila Wilaya haifanyi kazi kwa sababu ya kujengwa chini ya kiwango. Tatizo kubwa ni kama ilivyoelezwa katika swali la msingi mabomba yanavuja. Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuja Karatu ili ajionee mwenyewe jinsi wananchi na Serikali walivyojumia lakini pia akae na Halmashauri ili kuona ni namna gani miradi hiyo inafufuliwa? Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kama nilivyosema maeneo mengi hasa ya vijijini miradi mingi iliyotekelizwa ilitekelezwa chini ya viwango. Wameweka mabomba ambayo yako chini ya viwango, wameweka valve ambazo ziko chini ya viwango. Sisi tunahakikisha kwamba sasa tatizo hili linamalizika na pale ambapo mkandarasi ameweka vifaa ambavyo viko chini ya viwango anatakiwa aviondoe na afanye kazi hiyo na aweke vifaa ambavyo vina viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekubaliana na Mheshimiwa Mbunge tutakwenda tutaona tatizo hilo na tutalitatua kwani nia ya Serikali naendelea kusema tena ni kuhakikisha kwamba tunawapelekea wananchi maji safi na salama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Deo Ngalawa.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wananchi wa Jimbo la Ludewa huwa wana kawaida ya kujiongeza. Miradi mingi ambayo inafanyika kwenye Jimbo la Ludewa wananchi wanakuwa wameianza kabla ya Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni shahidi alipofika maeneo ya Mlangali alishakuta watu wameshajichangisha shilingi milioni 90 na wakawa wanaionomba Serikali shilingi milioni 50 kwa ajili ya kumalizia. Niishukuru Serikali ilitupa ile hela. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna miradi mbalimbali inaendelea kwenye Kata ya Mavanga na Ludewa Mjini. Je, Serikali ipo tayari kutusaidia na kuhakikisha mfano miradi ile ya Ludewa Mjini, Iwela na Lifua inakamilika katika kipindi kifupi iwezekanavyo? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kawaida nia ya Serikali ni kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama na kwa muda mfupi. Kwa hivyo, nitahakikisha kwamba miradi ya Ludewa Mjini na maeneo mengine aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge tutatekeleza kwa muda mfupi ili Watanzania wa maeneo yale na maeneo mengine yote Tanzania waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ruth.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni miaka zaidi ya 50 ya Uhuru lakini maeneo mengi ya wafugaji bado wanakunywa maji kwenye mabwawa pamoja na wanyama, binadamu wanachota maji, wanyama pia wanakunywa hapo. Nimeona hili Mkuranga Kijiji cha Beta, nimeona hili juzi Monduli katika Kata ya Nararami. Kwa nini hii shilingi milioni 50 iliyotolewa kwa kila kijiji isitumike kwenda kuchimba visima

virefu katika yale maeneo ambayo hakuna maji na binadamu wanakunywa maji kwenye mabwawa na wanyama? (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa MwenyeKITI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ruth, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa MwenyeKITI, tunaelewa kwamba maeneo mengi ya nchi yetu yana changamoto kubwa ya maji, mijini na vijiji. Serikali tumejipanga vizuri, kwa mfano tu, juzi tumepata mkopo wa bei nafuu kutoka Benki ya Dunia ambapo tumepata takribani shilingi za Kitanzania bilioni 800 na pesa nydingi kati ya hizo zitapelekwa vijiji kutatua changamoto ya maji kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema. Siyo hivyo tu, kwenye bajeti yetu hii ya mwaka huu tuna takribani shilingi bilioni 630 kwa ajili ya kupeleka maji vijiji. Nataka niwahakikishie Watanzania kwamba Serikali tumejipanga na kila kijiji tutawapelekea maji safi na salama.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mbunge wa Kigoma Kusini.

Na. 115

Miradi ya Maji Jimbo la Kigoma Kusini

MHE. HASNA S. K. MWILIMA aliuliza:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu miradi ya maji ya Kali, Rukoma, Ilagala, Kandego, Uvinza na Nguruka ambayo wakandarasi wamesimama kwa ukosefu wa fedha?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna Sudi Katunda, Mbunge wa Kigoma Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji Awamu ya Kwanza chini ya Mpango wa Vijiji 10 kwa kila halmashauri, Miradi ya Maji ya Rukoma na Kandaga ilitekelezwa katika Halmashauri ya Kigoma na miradi ya maji katika vijiji vya Kalya, Ilagala, Uvinza na Nguruka ilitekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli wakandarasi wa miradi hiyo walikuwa wamesimama kutokana na changamoto ya kifedha. Katika bajeti ya mwaka 2017/2018, Serikali tulitumia kiasi cha shilingi bilioni 1.01 katika Halmashauri ya Uvinza kwa ajili ya kuendelea kukamiliisha miradi ya maji ambayo hajakamilika ikiwemo miradi ya Kayla, Ilagala, Uvinza na Nguruka. Aidha, Halmashauri ya Kigoma ilitumia jumla ya shilingi bilioni 581.2 kuendelea kukamiliisha miradi ya maji vijijini ikiwemo Rukoma na Kandaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 2.8 na shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya Halmashauri za Wilaya ya Uvinza na Kigoma mtawalia ili kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maji. Aidha, halmashauri zote nchini zimeshauriwa kuwasilisha kwa wakati hati za madai ya wakandarasi wanaojenga miradi ili ziweze kulipwa mapema iwezekanavyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hasna.

MHE. HASNA S.K. MWILIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini tumekuwa na tatizo kubwa la wakandarasi hawa, kwa mfano, Mradi wa Nguruka Mheshimiwa Rais alifanya ziara tarehe 23 Julai, 2017 akatoa tamko hadi Desemba. 2017 Mradi wa Nguruka uwe umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa zinaletwa na Serikali wakandarasi hawa hawakamilishi miradi hii na mradi wa Nguruka wananchi wanaona pesa zinaingia lakini hawapati maji. Mradi wa Uvinza pesa zinaletwa lakini wakandarasi hawakamilishi ili wananchi wapate maji. Mradi wa Kandaga Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi tarehe 17 Julai, 2018 tulifanya ziara pale ukampa mkandarasi wiki mbili lakini hadi leo hii hakuna maji yanayotoka pale. Swali langu la kwanza, je, Serikali ina kauli gani kwa hawa wakandarasi ambao wanalipwa pesa lakini hawakamilishi miradi kwa wakati? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, tarehe 29 Julai, 2018, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara kwenye Kijiji cha Mwakizega na wananchi wakamlilia kwamba tunahitaji maji na tamko tukaambiwa tuandae taarifa ya mradi wa maji ili tuweze kuwasilisha Wizarani. Hivi navyoongea Injinia wa Maji Halmashauri ya Uvinza yuko hapa Dodoma ameshawasilisha andiko hilo la mradi ambalo linagharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.9. Je, ni lini sasa Wizara itatuletea pesa ili tuanze kutekeleza huu mradi mpya wa Mwakizega? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya maswali hayo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hasna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kwamba Serikali inachukua hatua gani kwa wakandarasi ambao wanashindwa kukamilisha kazi kwa wakati. Kuna taratibu mbalimbali Serikali inachukua kama mkandarasi anashindwa kukamilisha kazi kwa wakati. Hatua ya kwanza, kama mkandarasi anachelewesha kazi tunampiga faini kutokana na ucheleweshaji na kila siku mkandarasi huyo analipa faini inategemeana na mradi wenywewe na kiasi cha gharama za mradi. Hatua ya pili ambayo kama mkandarasi atashindwa kutelekeza kazi kwa wakati tunaweza kumfutia usajili na

mwisho wake hatoweza kufanya kazi yoyote ya ukandarasi kwenye sekta zote za ujenzi pamoja maji na sekta zote hapa nchini. Tutawasimamia wakandarasi wote tuhakkishe kwamba wanafanya kazi kwa wakati na wanazimaliza kwa wakati ili Watanzania ambao wamesubiri maji kwa muda mrefu waweze kupata maji na salama kwa muda unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge amezungumzia kuhusu andiko, andiko tumelipokea na kama kawaida andiko lolote lazima lipitie michakato mbalimbali. Mara litakapokamiliika tutaweza kutoa fedha ili mradi huo uweze kutekelezwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka na Mheshimiwa Kitandula.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko mradi ambao unataka kutekelezwa kwenye Mji wa Tunduma na *SADC* na Mheshimiwa Waziri katika Bunge liliopita alisema kwamba ameshampeleka *consultant* pale. Wananchi wa Tunduma wanataka kujua mpaka sasa mradi umefikia kiwango gani katika maandalizi ya utekelezaji?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Tunduma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli *consultant* ameenda kwa ajili ya mradi huo lakini taratibu za utekelezaji zinakwenda hatua kwa hatua. Kwanza *consultant* anakwenda kufanya *study* analeta hiyo *study* tutaipitia baadaye kama pesa ipo utafuata mchakato wa kutafuta mkandarasi ili aweze kufanya kazi hiyo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kitandula.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu wa Mradi wa Kupeleka Maji Makao Makuu ya Wilaya ya Mkinga kutoka Mto Zigi kuelekea Horohoro lakini mpaka sasa hakuna dalili yoyote ya jambo hili kufanyika. Ni lini usanifu huu utaanza?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba usanifu huo utaanza mara moja, tunajipanga kuhakikisha kwamba tunatafuta wataalam ili wakafanye kazi hiyo.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoaa Mjini, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Felister Bura.

Na. 116

**Miundombinu ya Chanzo Kikuu
cha Maji cha Chemchem Kondoaa**

MHE. FELISTER A. BURA (K.n.y. MHE. EDWARD M. SANNDA) aliuliza:-

Mtando wa miundombinu ya usambazaji wa maji toka chanzo kikuu cha maji ya chemchem katika Jimbo la Kondoaa Mjini ni ya zamani na chakavu. Katika ziara yake mwaka jana, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kutupatia fedha za ukarabati wa miundombinu hiyo:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu ya swali hilo.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Edwin Sannda, Mbunge wa Jimbo la Kondoaa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uchakavu wa miundombinu ya usambazaji maji katika chanzo kikuu cha maji ya chemchem katika Jimbo la Kondoaa Mjini. Serikali imekwishafanya tathmini ya awali ya ukarabati wa chanzo hicho unaokadiriwa kugharimu kiasi cha shilingi billioni 4.1. Ukarabati wa chanzo hicho unatarajiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza kuboresha huduma ya maji kwa wananchi wa Jimbo la Kondoaa Mjini, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali kuitia Hal mashauri ya Mji wa Kondoaa ilikamilisha uchimbaji wa visima vinne vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 2.6 kwa siku. Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa maji kutoka kwenye visima hivyo unaendelea. Kazi zinazotekelze wa ni pamoja na ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 9.912, ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji yenye urefu wa kilomita 30.172 na ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 33. Kukamilika kwa mradi huo kutawanufaisha wakazi wapatao 13,191 wa maeneo ya mitaa ya Kwapakacha, Bicha, Kilimani, Kichangani na Tura.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Felister.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwanza tunaishukuru Serikali kwamba tumechimbiwa visima vinne kuitia Hal mashauri ya Mji wa Kondoaa. Pamoja na visima hivyo ambavyo vimechimbwa bila ukarabati wa

miundombinu ya maji, uchimbaji wa visima hivi havitawasaidia sana wananchi wa Kondoa Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo katika bajeti iliyopita tuliomba fedha kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu hiyo. Naomba kujua Serikali imetenga fedha kiasi gani kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya zamani ukizingatia kwamba maeneo kama Kwapakacha, Kilimani na Bicha katika uchimbaji wa visima hivyo kuna maeneo watatumia miundombinu ya zamani? Je, Serikali iko tayari kujenga baadhi ya miundombinu ili wananchi wa Kondoa Mjini wapate maji? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa ahadi ya ukarabati wa miundombinu ya maji katika Mji wa Kondoa ni ya ahadi ya viongozi wa Kitifa na hasa walitembelea Kondoa Mjini mwaka jana akiwemo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Je, ahadi hizo zitatekelezwa lini? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, swali la takwimu litakuwa la tatu unaweza kuliacha maana ameuliza maswali matatu Mheshimiwa.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyosema mara nyingi, nia ya Serikali ni kuhakikisha kila eneo tunapeleka maji safi na salama. Kwa upande wa Kondoa Mjini sasa hivi tuna mradi ambao utahakikisha kwamba tunapeleka maji kila eneo la Kondoa Mjini ambapo kama nilivyosema kwenye swali la msingi kwamba sasa hivi tunajenga miundombinu ya kilomita 9.12, tunajenga miundombinu ya kusambaza maji kilomita 30.172 kwa sababu kuchimba visima ni jambo lingine na kuweka miundombinu ni jambo linguine. Kwa kulijua hilo, Serikali tunaendelea sasa hivi kujenga miundombinu hiyo tuhakikishe mwananchi kila eneo anapata

maji safi na salama. Tunategemea mradi huu utamalizika hivi karibuni na wananchi watapata maji hayo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nsanzungwanko na Mheshimiwa Komu.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mji wa Kasulu ni kati ya miji ambayo inasubiri kwa hamu sana fedha za mkopo wa India katika ile miji 17. Hii ni kwa sababu Mji wa Kasulu unakabiliwa na tatizo la maji na hata machache yaliyopo ni machafu, kwa hiyo, kutibu tatizo hilo ni fedha za Mfuko wa India. Sasa niapenda kujua miradi hiyo 17 inaanza lini ikiwa ni pamoja na Mji wa Kasulu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Kasulu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuna mradi mkubwa wa India ambapo siyo miji 17 sasa itakuwa miji 25 na mradi huo utagharimu shilingi za Kitanzania trilioni 1.2. Tenda ya kwanza ilitangazwa tarehe 17 Agosti, kwa ajili ya *pre-qualification* na *consultancy* na itafunguliwa tarehe 17 Septemba. Kwa Mheshimiwa Mbunge ye yeyote anayehitaji kujua *information* za mradi huu anaweza kupata kwenye website ya Benki ya Exim ya India. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Komu.

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Moshi Vijijini hali iko kama Kondoa, miundombinu mingi imejengwa siku nyingi na imechakaa. Kwa kutambua hilo, Mamlaka ya Maji

(MUWSA) imefanya kazi kubwa ya kukarabati miundombinu hiyo katika Kata mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kulikuwepo na mradi mmoja katika Kata ya Mabogini ambao ilikuwa inahusu vijiji vinne na Wizara ilipokuja kuzindua kwa kuona kazi kubwa iliyofanywa na MUWSA katika Kata zingine iliahidi kutoa shilingi bilioni 1.8 kwa ajili ya kuendelea kusambaza maji kwenye vijiji vingine vitano vya Mvulei, Muungano na Msarikia. Nataka kujuua ni lini fedha hizo zitapelekwa MUWSA ili waweze kutekeleza ahadi hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo kwa ufupi.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Komu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na ye ye kwamba MUWSA inafanya kazi nzuri na tunawapongeza sana na tumewapa miradi mingi kwa ajili ya Moshi Vijiji na wanafanya kazi kubwa. Serikali tuko tayari wakati wowote wakituletea, kwa sababu tumeshawapa kibali cha kupeleka mkandarasi kuanza kufanya kazi hiyo na wakati wowote watakapoleta *certificate* kwa ajili ya malipo ya mkandarasi sisi tumejipanga vizuri na tutaweza kuwalipa ili kazi hiyo iendelee. Mheshimiwa Mbunge naomba uwasiliane na MUWSA kujuua wamefikia wapi lakini sisi tuko tayari fedha tunayo wakati wowote tutaweza kuwalipa waendelee na kufanya kazi hiyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Swali la mwisho, Mheshimiwa Mftaha kwa ufupi kabisa.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mtwara Mjini kuna Mradi wa Maji ambao unatekelezwa na Serikali kutoa maji Kijiji cha Lwelu kuelekea Kata za Ufukoni, Magomeni na maeneo mengine ya Mtwara Mjini lakini mkandarasi yule anasuasua sana na tayari kasha-

rise certificate Wizara bado haijamlipa na mradi umesimama. Je, Serikali inatoa kauli gani ili kuhakikisha mkandarasi yule analipwa na mradi ule unaendelea haraka ili wananchi wa Mtwara Mjini wapate maji? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, kauli tu ya Serikali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tuna miradi mingi hapa nchini inaendelea na huu mradi wa Mtwara tunaufahamu vizuri na kila mwezi sisi tunaendelea kulipa, hata leo tunafanya malipo kwa wakandarasi. Tutahakikisha kwamba na mkandarasi huyo tunamlipa ili aweze kuendelea kumaliza kazi hiyo illi wananchi wa Mtwara Mjini waweze kupata maji safi na salama. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa majibu mafupi na mazuri. Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 117

Kupeleka Umeme katika Kata za Jimbo la Mufindi Kusini

MHE. MENDRAD L. KIGOLA aliuliza:-

Serikali imekuwa na mpango kabambe wa kupeleka umeme vijijini:-

Je, ni lini Serikali itawapelekea umeme wananchi wa Kata Itandula, Nyololo Shuleni, Maduma, Uдумка, Kilolo, Kiowole na Idete?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji kupitia Wakala wa Nishati Vijiji (*REA*), Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza kuanzia Julai, 2017 hadi Juni 2019. Katika Wilaya ya Mufindi jumla ya vijiji 53 vitapatiwa umeme kupitia mradi huu unaotekelwa na mkandarasi Kampuni ya *Sengerema Engineering Group Limited* aliyepewa kazi za mradi huo kwa Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mufindi Kusini, mradi utapeleka umeme katika Kata za Makungu, Igowole, Mninga, Nyololo, Isalavanu, Mbalamaziwa na Kasanga ambapo Vijiji vya Lugolofu, Mukungu, Lugema, Ibatu, Kisasa, Makalala, Ikwega, Itulituli, Lwing'ulo, Njojo, Nyololo Shuleni, Mjmwema, Idetero, Kimandwete, Ukemele, Udomuka, Lyang'a, Kilolo, Ihomasa pamoja na Maduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi katika Wilaya ya Mufindi zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 139.63, njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 170, ufungaji wa transfoma 85 za kVA 50 na 100, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 2,596. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 11.92. Kwa sasa mkandarasi ameshasimika nguzo za umeme wa *line* kubwa za HT kwa asilimia 90 na nguzo za umeme wa *linendogo* LV kwa asilimia 95 kwa jimbo la Mufindi Kusini. Kazi ya ufungaji transfoma na kuanganisha wateja itaanza mwishoni mwa Septemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vingine vya Kata ya Itandula, Kiyowole na Idete vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa mradi wa REA III unaotarajia kuanzia Julai, 2019 na kukamilika Juni, 2021. Ahsante.

MWENYEKIT: Mheshimiwa Kigola.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na nitoe pongezi kwa mkandarasi ambaye amepangwa kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kwa kazi nzuri anayoifanya. Tulikuwa tuna tatizo la transfoma pale lhowanza baada ya kumpa taarifa nimepata taarifa kwamba ameshaipeleka na pale Mbalamaziwa tulikuwa tuna tatizo la transfoma ameshaipeleka na sasa hivi mkandarasi yupo *site*. Kwa kazi hiyo nzuri, naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza kuna vitongoji vingi sana kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini ambavyo havikufanyiwa *survey* na tulikuwa tumeandika hata majina tukapeleka pale TANESCO, je, vile vitongoji ambavyo vilikuwa vimerukwa mara ya kwanza na vyenyewe vitapewa umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ningemuomba Waziri kama atapata nafasi kwa sababu kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini hawajaja, je, atakuja sasa kufanya m kutano akielezea vizuri matumizi haya ya umeme?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumepokea pongezi za Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo miradi ya REA III inavyoendelea katika Wilaya ya Mufindi hususani katika jimbo lake. Namshukuru kwa kulithibitishia Bunge lako kama mkandarasi yupo anaendelea vizuri na kweli mkandarasi Sengerema ni mionganini wa wakandarasi ambao wanafanya kazi zao vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimpongeze yeye mwenyewe Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala ya nishati katika jimbo lake, anafanya kazi vizuri. Ndiyo maana katika maswali yake ya nyongeza amekiri kwamba kulikuwa na tatizo la transfoma kwenye kata alizotitaja na kutokana na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri transfoma hizo zimeshafika katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake moja ameuliza ni lini vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme vitapata? Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inaendelea kufanya upembuzi yakinifu kwenye Mradi wa *densification II* baada ya kufanikiwa kwa *densification I*, ambayo itahusisha mikoa 17 pamoja na Mkoa wa Iringa na katika vitongoji ambavyo vistasalia vitapatiwa umeme katika mradi wa ujazilizi awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kutembelea katika Jimbo lake la Mufindi Kusini na hususan Wilaya ya Mufindi, nataka nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya Bunge hili kwa kweli tutatembelea Mkoa wa Iringa kwa sababu mpaka sasa hivi tuna vijiji takribani 20 vinatakiwa kuwashwa umeme lakini pia kuna mradi ambao unaendelea wa *BTIP* ambao kwa kweli umefanya vizuri. Hivyo, nataka nilitaarifu Bunge ipo kazi ya kufanya katika huo Mkoa wa Iringa na Jimbo lake la Mufindi Kusini, kwa hiyo, tutakuja. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwamoto na Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nichukue nafasi hii nimpongeze Naibu Waziri pamoja na Waziri husika kwa kazi nzuri ambayo mnafanya ya kuhakikisha wananchi wanapata umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aliwahi kufika baadhi ya vijiji kikiwemo Kijiji cha Kihesa Mgagao na umeme tayari umeshafika. Naomba awaondoe wasiwasi

wananchi wa sehemu umeme umefika hasa vitongoji kwamba umeme watapata au hawatapata?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna Kata za Ukwega, Kising'a, Nyanzwa, Udekwa na Winome hawajapata umeme haujapimwa kabisa. Naomba niulize ni lini wataenda kupimiwa ili nao wawe na uhakika wa kuingia kwenye nchi mpya ya viwanda?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kweli mradi wa REA III unaendelea vizuri na umeshaanza katika mikoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwamoto, napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwamoto anavyofuatilia masuala ya umeme katika Jimbo lake la Kilolo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilifika katika Jimbo la Mheshimiwa Mwamoto na kijiji cha Nghuruwe pamoja na Kihesa Mgagao kulikuwa na changamoto kubwa sana. Kijiji cha Nghuruwe kilishapata umeme na sasa wanaendelea kupeleka umeme katika Kijiji cha Kihesa Mgagao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mwamoto kabla ya mwezi huu kuisha vitongoji vyote vya Kijiji cha Kihesa Mgagao vitakuwa vimeshawashwa umeme. Kadhalika bado vitongoji vyake saba katika maeneo ya karibu na Kihesa Mgagao, navyo tutavitembelea wiki ijayo namhakikishia kwamba na vyenyewe vitapata umeme kabla ya mwisho wa mwezi ujao. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Juma Nkamia.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Chemba kwenye Kata za Kidoka, Jangalo na Msaada pamoja na maeneo ya vijiji vyake, kumekuwa na nyaya za umeme kwa muda mrefu lakini tatizo lililopo sasa ni kuwasha tu. Je, Serikali inanipa majibu gani ya uhakika kwamba ni lini maeneo haya yatapelekewa transfoma ili kuwasha umeme katika maeneo hayo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Nkamia anavyofuatilia masuala ya umeme katika Jimbo lake la Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpe taarifa Mheshimiwa Nkamia, nivyoongea hivi sasa transfoma tatu zinakwenda katika Kijiji cha Kidoka kwa ajili ya kuwasha umeme, lakini kesho pia wataendelea kupeleka nguzo pamoja na transfoma na nyaya katika Kijiji cha Msaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Jangalo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tushirikiane baada ya vijiji hivi kuwashwa tutaendelea na Kijiji hicho. Wakati kazi hizo zinavyoendelea kule Kwa Mtoro nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge yapo magenge sita yanafanya kazi hivi sasa ili na yenyeWE kabla ya mwisho wa mwezi wa kumi iweze kuwashiwa umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Nkamia anavyoshirikiana na Serikali. Ahsante.

MWENYEKITI: Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto.

Kata ambazo Hazikupata Umeme wa REA III – Lushoto

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Kata za Gare, Kwai, Kwemashai, Makanya, Kilole, Ngwelo na Ubiri hazikufikiwa na REA III mpaka sasa:-

Je, ni lini sasa Serikali itafikisha umeme kwenye kata hizo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaji Shaabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Miradi ya Kupeleka Miradi ya Umeme Vijiji kuititia Wakala wa Nishati (REA). Mradi wa REA III mzunguko wa kwanza ulianza Julai, 2017. Vijiji vitakavyopelekewa umeme kwenye Jimbo la Lushoto ni pamoja na Magamba, Kwegole, Kwehungulu, Kwebarabara, Maboi, Milemeleni, Kungului, Shume A, Makunguru, Shume B, Ngazi, Mhezi, Kwezindo, Kweboi, Nkelei, Viti, Langoni B, Vuli A na Kwemakulo, Mradi huu unatarajia kukamilika Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya mradi huu zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 5.67, njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 46, ufungaji wa transfoma 23 za 50 kVA pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 520. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 1.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Kata ya Gare, Kwai, Kwemashai, Makanya, Kilole, Ngwelo na Ubiri vitapatiwa umeme katika mzunguko wa pili wa mradi wa REA III utakaoanza Julai, 2019 na kukamilika Juni, 2021. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Shekilindi.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu pia niendelee kumpongeza Waziri Kalemani na Naibu pamoja na timu yake kwa kutuma wataalam kuja ku-survey katika Kata za Kwekanga, Mbwei, Migambo, Nguli, Lushoto, Magamba na Mlola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, je, pamoja na ku-survey kata zote hizo hizo pamoja na alilozitaja, ni lini sasa wananchi wangu watakuja kupimiwa hawa ili wawewe kupata umeme kwani umeme ni huduma ambayo walikuwa wanaisubiri kwa muda mrefu sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mkandarasi aliyepewa kazi ya kujenga umeme katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto tokea mwaka jana mpaka leo hii amejenga kitongoji kimoja tu ambacho ni cha Magamba Mabughai. Hii inaonyesha uchelewaji mkubwa sana, je, Serikali haioni sasa kuwa kuna haja ya kubadilisha mkandarasi huyu kuweka mkandarasi mwingine ambaye anaendana na kasi ya hapa kazi tu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Shekilindi anavyofuatilia masuala ya umeme katika Jimbo lake la Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunakubali kupokea pongezi kwa kazi nzuri zinazofanywa na sehemu nyingine ya mkandarasi lakini zipo changamoto kweli kwa mkandarasi na nimeongea na Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nilikuwa

nimempa vijiji vinne tu kati ya vijiji kumi na mbili, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Lushoto tumemuongezea vijiji vingine vinane vipyta ambavyo vimeshafanyiwa *survey* na mkandarasi anaanza kuvifanyia kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu lini vitapelekewa umeme, tunapoongea hapa mkandarasi ameshaweka magenge mawili, anaendelea na usambazaji wa nguzo pamoja na kufunga nyaya katika Kijiji cha Magamba pamoja na Mabughai. Kwa hiyo, ni matarajio yetu kwamba ndani ya mwezi huu wataviwasha vijiji hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la pilli la uwezo wa mkandarasi, ni kweli mkandarasi huyu alianza kwa kususasua lakini tumeshakaa naye na ameshaweka magenge kumi na mawili kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge ni matarajio yetu mbali ya kumbadilisha tutamsimamia, tutamshinikiza, tutahakikisha kwamba anafanya kazi na anakamilisha ndani ya wakati.

MWENYEKITI: Umeme upo vizuri Waheshimiwa, maswali naomba yawe kwa ufupi, Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Almas na Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RASHID R. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Mimi naona wivu wenzangu wanapotoa pongezi kwamba maeneo yao umeme umeshapatikana, sasa mimi nina masikitiko makubwa kwamba bado katika Jimbo la Mlalo, Halmashauri hiyo hiyo ya Lushoto, kata nne bado umeme haujawaka katika Kata za Mbalamo, Shagayu, Mbalu na Hemtoe. Barua ya kutoka REA kwenda kwa mkandarasi imetoka tangu mwaka jana. Nataka Mheshimiwa Waziri anipe *commitment* ni lini katika kata hizi na zenyewe umeme utawaka katika Jimbo la Mlalo, Halmashauri ya Lushoto?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Shangazi kwa maswali yake mazuri na kweli naungana na yeye kwamba kati ya maeneo ambayo mkandarasi alikuwa hajaanza kazi rasmi ni pamoja na Jimbo la Mheshimiwa Shangazi. Tunapoongea hapa na leo asubuhi tumeongea na Mheshimiwa Shangazi na mkandarasi ameshapeleka makundi manne, ni matarajio yetu atafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimuahidi Mheshimiwa Shangazi kwa niaba ya wananchi wake, mimi baada ya Bunge hili kuisha Mheshimiwa Shangazi tutafuatana mimi na naye tutakwenda kusimamia mguu kwa mguu mpaka vijiji vyake vyote ambavyo havijapatiwa umeme sasa vitapatiwa umeme. Awape uhakika wananchi wake kwamba Serikali hii haina mchezo kwenye suala la umeme vijijini.

MWENYEKITI: Safi kabisa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Maige.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kuniruhusu niulize hili la nyongeza, lakini kwanza nianze na shukurani kubwa sana, Mheshimiwa Waziri wa Nishati alikuja jimboni kwangu kuzindua *REA* ///. Naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri kwa nini mkandarasi hajaanza kazi kwenye barabara ile ya kuja nyumbani kwangu, kijiji cha kwetu Kasenga, Majengo, Ikongolo, Kanyenye na Nzubuka?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Maige kwa swalı lake la nyongeza. Kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Maige, ameshafanya vijiji kumi na viwili kwenye jimbo lake lakini vijiji vya barabara ndiyo anaendelea navyo. Kwa hiyo, ni shauku ya Mheshimiwa Maige na wananchi kwamba vijiji vyote vingepatiwa umeme kwa siku moja. Nimhakikishie Mheshimiwa Maige kwamba hivi sasa anaendelea na Kijiji cha Lipogolo na kuna Kitongoji kinaitwa Kwa Muni ndipo anakosimika nguzo. Kwa hiyo, niungane na Mheshimiwa

Mbunge kwamba ameshamaliza vijiji vya ndani sasa ameanza kufanya kazi katika vijiji vya kandokando mwa barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Maige vijiji vyake kumi na moja vilivyobaki, vyote vitapelekewa umeme katika *round hii* ya kwanza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Tarehe 11 Julai, 2017, narudia tarehe 13 Julai, 2017 Mheshimiwa Waziri alikuja Nyamatala kuzindua umeme Kimkoa na uzinduzi ulifanyika katika Kijiji cha Nyamatala hadi leo ni kijiji kimoja tu ambacho kimeshawashwa umeme lakini kisingizio wanasema hakuna nyaya, nguzo na transfoma. Naomba majibu ya Serikali, hivi vijiji ambavyo vilikuwa vimepangwa kuwashwa umeme vitawashwa lini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Ndassa na kwa kweli niseme tu katika Mkoaa mzima wa Mwanza nitoe marekebisho kidogo ya hoja ya Mheshimiwa Ndasa, ni vijiji 21 tayari vimeshawashwa umeme siyo kijiji kimoja. Ni kweli kabisa katika Jimbo lake Kijiji cha Nyamatala ambapo tulifanya uzinduzi tayari kimeshawashwa umeme na sasa wanaendelea na kijiji kinachofanya kwenda Sangabuye. Nikubaliane na Mheshimiwa Ndassa kwamba *speed* ya mkandarasi haikuwa nzuri, lakini tangu wiki iliyopita ameshaleta nguzo 500 katika Jimbo lake ni matarajio yetu kwamba sasa *speed* itaongezeka. Nimwombe Mheshimiwa Ndassa tushikiriane atuletee maeneo yenye changamoto ili kazi iianze kutekelezwa haraka iwezekanavyo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, najua wengi mna maswali ya umeme lakini muda wetu hauruhusu, tumwamini Mheshimiwa Waziri na Naibu wake wako vizuri, naamini tukija Bunge lijalo maswali yatapungua. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Yahya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni, sasa aulize swali lake.

Na. 119

Asilimia 70 Inayochukuliwa Mtu Anapokata Mti

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza:-

Mjasiliamali au mtu ye yeyote anapokata mti anatakiwa achukue 70% ya kile anachokilipia:-

- (a) Je, ni lini *recovery rate* ya 30% ya mbao ilifanyiwa utafiti?
- (b) Je, ni taasisi gani ilifanya utafiti huo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya miti ya Serikali kwa ajili ya kuvuna hufanya baada ya kufanya tathmini ya ujazo wa miti kwa kupima unene na urefu wa miti inayotarajiwa kuuzwa. Ujazo huu hauhusishi ujazo wa matawi, majani na mizizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zilizowahi kufanywa na wataalam wetu wa misitu kati ya mwaka 1996 hadi 1999 wakati wa kutekeleza Mradi wa FRMP (*Forest Resource Management Programme*), zilibainisha kuwa mteja anaweza kupata mbao kati ya asilimia 60 – 70 ya ujazo wa mti uliopimwa kama atachakata magogo hayo kwa kutumia

mashine zenyе ufanisi wa kiwango cha juu ambazo ni *frame saw* au *band saw*. Mashine hizi hupatikana kwenye viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika viwanda vidogo vidogo na vya kati ambavyo hutumia mashine zenyе ubora wa chini kiwango cha uzalishaji ni kati ya asilimia 20 - 43 ambapo wastani ni asilimia 30 ya ujazo wa mti. Utafiti huu ulifanywa kati ya mwaka 2005 na 2007 na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na Chuo cha Viwanda vya Misitu cha Moshi (FITI). Teknolojia duni, uelewa mdogo na usimamizi hafifu ndiyo chanzo cha kuwa na ufanisi huo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia utafiti huo na ufanisi wa teknolojia iliyopo sasa ya msumeno wa mkono na msumeno wa duara (*circular saw*) hauwezi kuzalisha mbao zenyе ujazo wa zaidi ya asilimia 30 ya ujazo wa mti uliopimwa. Kiwango cha asilimia 30 kitaalam tunakiita *recovery rate*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Massare na Mheshimiwa Gekul.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, tofauti ya majibu haya kwamba kuna asilimia 60 na 70 na kuna asilimia 30, wadau hawa wanapita katika njia moja na wanachukua vibali sehemu moja na wakaguzi wa vizuia, wanakagua bila kujua huyu katoka kwenye mashine ya kisasa au mashine ya kizamani. Kwa mpango huo, inamaanisha kwamba kuna mwanya mkubwa sana wa rushwa, kuna mtu atatoka na asilimia 60 na mwingine asilimia 30. Je, sasa Serikali inakuja na mkakati gani uliobora kabisa kuepusha watumishi ambao sio waaminifu kufanya kazi ambayo imenyooka kwa dhamira

Iliyopo sasa ya Awamu hii ya Tano kwamba tunataka wananchi watendewe haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini sasa Serikali itaona njia bora zaidi ya kusaidia wadau hawa wajasiriamali, wale ambao wana mashine za kizamani waweze kuwezeshwa na kupata mashine hizi za kisasa ili kuondoa mkanganyiko huu ambao unasababisha mwanya mkubwa wa rushwa?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi kwa maswali hayo mawili ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omari Massare, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza kwa sababu yeye ni mdau mkubwa sana wa mazao yatokanayo na misitu na kwa kweli amekuwa akifanya kazi nzuri sana na amekuwa mshauri mzuri sana katika masuaa mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati ambao Wizara imeweka, Serikali kwa kweli imeweka mkakati mkubwa wa kuhakikisha tunawahamasisha wananchi wote wahakikishe wanapata teknolojia za kisasa, mashine ambazo ni bora kwa sababu hizi mashine zingine kwa kweli zinafanya upotevu mkubwa sana na hasara ni kubwa. Katika suala hilo ndiyo maana tumeweka mkazo kwamba wale wote ambao wanakuwa na zile mashine ambazo zinapoteza sana kwa kweli hawaruhusiwi. Pale ambapo itabainika kwamba baadhi ya watumishi wetu katika maeneo kadhaa wanaruhusu hizo mashine zitumike kwa rushwa basi tunaomba mtusaidie kututajia majina ili hatua kali ziweze kuchukuliwa kwa watumishi wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu namna ya kuwasaidia Watanzania hawa, kwa kweli ziko njia nyingi za kuwasaidia Watanzania lakini nitumie nafasi hii

kuwahamasisha kwamba wajaribu kutafuta mikopo ya aina mbalimbali. Kuna aina nyingi za mikopo sasa hivi, kuna ile mikopo inayotolewa na Halmashauri, kuna mifuko mingi inatoa mikopo basi wachukue mikopo ili waweze kupata mashine ambazo ni bora ambazo zitawafanya wapate mazao mengi zaidi kuliko mashine ambazo ziko hivi sasa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Gekul, swali fupi la nyongeza.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kumekuwa na kauli ya Serikali kwamba kila Halmashauri wapande miti 1,500,000 kwa ajili ya kuhifadhi mazingira yetu. Nafahamu Wizara hii, Wizara ya TAMISEMI pamoja na Mazingira wanahuksika na hawa wana mbegu za miti mbalimbali. Kwa nini msione umuhimu wa kutoa miti katika Halmashauri zetu hiyo 1,500,000 ili tuipande na kuhifadhi mazingira kwa sababu mkitegemea Halmashauri watoe fedha, wanunue hiyo miti Halmashauri zetu hazina fedha, kwa nini msitupe hiyo miti 1,500,000 tupande?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pauline Gekul, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa ni sera ya Serikali kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinapanda miti angalau kila Halmashauri 1,500,000 lakini kumekuwa na upungufu wa miche ya kupanda. Hivi sasa kama Serikali tumechukua hatua kwa kutumia Wakala wetu wa Misitu kuhakikisha kwamba wanashirikiana na Halmashauri kwanza kwa kuwapatia mengi lakini katika maeneo mengi kuwapa miche ile ambayo tayari tumeshaiotesha ili kusudi zile Halmashauri ziende kufanya kazi ile ya kupanda katika maeneo mbalimbali. Siyo tu suala la kupanda lakini baada ya kupanda pia Halmashauri

zihakikishe kwamba zinailinda ile miti na kuhakikisha kwamba kweli inakua sio tu inapandwa halafu inaachwa.

MWENYEKITI: Waheshimiwa muda wetu unaendelea kwisha. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia sasa aulize swali lake.

Na. 120

Papa Aina ya Potwe

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Papa aina ya potwe (*whale shark*) ni samaki ambaye duniani kote anapatikana Australia na Tanzania katika Kisiwa cha Mafia tu:-

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango mkakati wa kumtangaza samaki huyo pamoja na vivutio vingine vya utalii kama vile *scuba diving* na *sport fishing* duniani ili kuvutia watalii nchini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, papa aina ya potwe (*whale shark*) anapatikana katika maeneo mbalimbali duniani hususan nchi zilizoko katika maeneo ya tropiki kama Australia, Taiwan, Pakistan, India, Ufilipino, Indonesia, Afrika Kusini, Kenya, Msumbiji na kwa Tanzania anapatikana katika Visiwa vya Mafia (Kilindoni), Pemba na Zanzibar. Samaki huyu ni mmoja kati ya samaki wakubwa sana duniani na uzito wake unaweza kufikia mpaka tani zaidi ya 20 na urefu kufikia zaidi ya mita nane na hivyo kuwa kivutio kikubwa cha watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kuptitia Bodi ya Utalii Tanzania inaendelea kutangaza vivutio vya utalii ndani na nje ya nchi viklwemo vivutio vya Wilaya ya Mafia ikijumuisha papa aina ya potwe kwa kutumia mikakati mbalimbali ya utangazaji kama vile vipeperushi; majarida mfano (Afrika Asilia, *Selling Tanzania*, *Tan Travel*, *Tanzania Explore Magazine* na *Tanzania Map*; tovuti yenyne anuani www.tanzaniatourism.com; mitandao mbalimbali ya kijamii mfano youtube, instagram, twitter, facebook; *Tanzania Tourism App* inayopatikana kwenye Google Play Store kwenye simu za mkononi aina ya *smart phone*. Vilevile, utangazaji hufanyika kwa kutumia maonesho mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wilaya inaendelea kubaini maeneo ya fukwe katika mwambao wa bahari ya Hindi kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za utalii kama vile kuzamia (*scuba diving*), kuogelea (*swimming*), michezo ya kuvua samaki (*sport fishing*), kupiga mbizi (*snorkeling*) na *sunbathing*. Aidha, Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wananchi hususan wavuvi ili kuwatunza samaki aina ya papa potwe. Hivi karibuni, Serikali itazindua studio ya utalii, channel ya utalii itakayokuwa chini ya Shirika la Utangazaji Tanzania (*TBC*) na utambulisho wa Tanzania (*Destination Branding*). Hatua hii itaongeza ufanisi katika kutangaza vivutio vya utalii vilivypo nchini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dau, swali la nyongeza.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, moja ya matishio ya samaki aina hii ni anapoingia katika mitego ya wavuvi huwa anajeruhiwa kwa sababu wao wanakuwa hawamli lakini anapata majeraha katika kumnasua kwenye zile nyavu. Matokeo yake kwa kuwa ngozi yake iko very delicate, akipata michubuko anakufa. Sasa kwa kuwa samaki huyu ni wa *season* anapatikana kuanzia miezi ya

mwanzo ya Septemba mpaka Machi, je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kutengeneza *quota system* ambapo msimu wa potwe maeneo ya Kilindoni anapopatikana papigwe marufuku ya kuvua samaki wengine ili kumnusuru samaki huyu kwa sababu huenda akaondoka Mafia? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, utalii katika Kisiwa cha Mafia una gharama kubwa sana. Kila mtalii anayeingia eneo la hifadhi ya bahari analazimika kulipa dola 24 kwa siku moja. Kutokana na ughali huu, inalazimisha baadhi ya watalii kuanza kushindwa kuja Mafia. Je, Serikali sasa ina mpango gani kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvubi kupunguza kiwango hiki cha *entrance fees* za kuingia maeneo ya *marine park* ili kuweza kuvutia watalii wengi kuja Kisiwani Mafia? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Uvubi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya kaka yangu Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau kama ifuatavyo;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utalii Mheshimiwa Hasunga kwa majibu mazuri ya msingi hasa pale aliposema anaitaka jamii iweze kushiriki kikamilifu katika ulinzi wa samaki hawa au papa huyu anayeitwa papa potwe ama pia ninachukua pongezi nyingi sana kwa kaka yangu Dau kwa kuwa mshirika mzuri wa kulinda rasilimali zetu za Taifa ambazo zimekuwa ni kivutio kikubwa cha watalii katika visiwa vyetu hivi vya Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala alilolisema la kuweka utaratibu maalum Wizara yetu tunalichukua ili kusudi sasa tuwe na wakati wa uvubi katika eneo la Kilindoni na kuna wakati ambapo tutazuia ili kuwapisha papa potwe waweze kustawi. Bila ya kufanya hivyo, papa potwe watahama Mafia na tutasababisha utalii wa papa potwe uweze kutoweka katika eneo hili la Mafia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili juu ya tozo mbalimbali ambzo zinachukuliwa na Wizara yetu kuitia kitengo chetu cha *MPRU* kwa maana ya hifadhi ya bahari na zile zinazokwenda Wizara ya Utalii, mimi naomba nimhakikishie kwamba sisi Wizara yetu ya Mifugo na Uvuu na Wizara ya Maliasili na Utalii tutakaa kwa pamoja na kufanya *review* ya hizi tozo na kodi hizi zinazohusika katiak utalii huu ili kusudi tuweze kuhakikisha kwamba watalii waweze kuvutika kwa wengi zaidi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Yussuf swali fupi la nyongeza.

MHE. YUSSUF HUSSEIN SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kidogo nimeguswa hapa. Huyu papa ni papa mmoja na hadhru mwanadamu na mara nyingi kwa kule kwetu sisi huwa mwezi Desemba wanatoka Somalia wanakuja zao mpaka wanakuja kupiga kambi Minai – Zanzibar wanakuwa kwa wingi sana na huyu papa huwa anawafuata wale *dolphins*. Mara nyingi huwa anawafuata wale *dolphins*, swali langu kwa Mheshimiwa Waziri, kipindi cha Desemba mpaka Februari wanakuja na kurudi ni kipindi ambacho tunaweza tukafanya utalii mkubwa sana katika eneo letu la kuanzia mpakani na Kenya Duga mpaka Zanzibar. Je, Wizara yako imejipangaje sasa kutumia fursa hii ambayo wale *dolphins* na huyu papa wanatangaza nchi yetu wenywewe, sisi tutumile tu hiyo fursa. Lini tutatumia hiyo fursa ya kujenga hoteli katika ukanda huo. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba katika kipindi hiki hawa potwe wanakuwa wengi sana katika maeneo haya au wanakuja katika maeneo haya. Pia kuna vivutio vingi sana ambavyo viro katika ukanda wa bahari yetu hasa katika fukwe zetu hizi za bahari ambazo tunaweza tukafanya na ndiyo maana Serikali sasa hivi iko mbioni katika kuhakikisha kwamba tunaanzisha mamlaka ya kusimamia fukwe zote za bahari kusudi tuweze kufaidika na huu utalii wa baharini

ambao tulikuwa hatujautumia kwa muda mrefu sana. Kwa hiyo, naamini katika hizi jitihada, pale ambapo zitakuwa zimekamilika na sheria itakapokuwa imeletwa hapa Bungeni basi hizi jitihada zitakuwa zimekwenda sambamba na hilo wazo la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili. Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala sasa aulize swali lake.

Na. 121

Kuanzisha Mkoa Mpya wa Kipolisi Kahama

MHE. EZEKIEL M. MAIGE aliuliza:-

Jeshi la Polisi kupitia /GPE Ernest Mangu ambaye alifanya ziara Wilayani Kahama mapema mwezi Agosti, 2016 alitangaza kuanzisha Mkoa mpya wa Kipolisi wa Kahama na Wilaya za Kipolisi za Msalala, Ushetu na Kahama; na wilaya hizo mpya za kipolisi zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa askari na vitendea kazi vyao hasa vyombo vyaa usafiri:-

(a) Je, ni watumishi wangapi wamepangwa Wilaya mpya ya Kipolisi ya Msalala?

(b) Je, Serikali iko tayari kusaidia vyombo vyaa usafiri hasa magari na pikipiki Wilaya ya Kipolisi ya Msalala?

(c) Je, Serikali imejipangaje kujenga ofisi za polisi wilaya na nyumba za makazi kwa askari katika Wilaya za Msalala, Ushetu na Kahama Mjini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji wa huduma ya kipolisi katika maeneo ya Ushetu, Msalala na Kahama. Aidha, maombi ya Msalala kuwa Wilaya ya Kipolisi yameshakamilika na maombi ya Kahama kuwa Mkoa wa Kipolisi yanaendelea kuzingatiwa. Kwa sasa Wilaya ya Msalala ina jumla ya maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali 57.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kuona kuwa vitendea kazi kwa Jeshi la Polisi vinapatikana ili kurahisisha utoaji wa huduma za polisi kwa wananchi. Wilaya mpya ya Msalala imepatiwa mgao wa gari moja jipyga na taratibu za usajili zitakavyokamilika gari hilo litapelekwa Msalala kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Msalala, Ushetu na kahama Mjini ni mionganini mwa wilaya 65 nchini ambazo hazina majengo ya vituo vya polisi vyenye hadhi ya wilaya. Hata hivyo, halmashauri ya wilaya imeshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa kituo na makazi ya askari na ujenzi utaanza mara pale fedha zitakapokuwa zimepatikana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Maige, swali la nyongeza.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na hasa hili la kukubali ombi la kutuletea angalau gari moja kwa ajili ya kusaidia shughuli za polisi. Pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kutambua kwamba Jeshi la Polisi lina idadi ndogo sana ya askari, wananchi wa Msalala pamoja na kanda nzima ya ziwa walishaanzisha utaratibu wa ulinzi wa jadi (Sungusungu) ambao ni askari wa kujitolea na husaidia sana shughuli za polisi kukabili matukio pale ambapo polisi wanakuwa hawajafika. Kwa bahati mbaya sana Wizara ya Mambo ya

Ndani na Jeshi la Polisi limekuwa likitoa ushirikiano mdogo sana kwa watu hawa ambao wanafanya kazi kwa kujitolea na mara nyingi wamekuwa wakiwa-harass pale tukio linapotokea badala ya kuwatafuta wahalifu wanakwenda kukamata wale viongozi wa Sungusungu na kuwalazimisha au kuwataka kwamba wasaidie kutaja au kutoa taarifa ambazo zingeweza kusaidia Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujuu Serikali au Wizara inachukua au ina mkakati gani wa kushirikiana na Jeshi la Sungusungu ili kusaidia jithada ambazo tayari zipo kwa sababu pia askari wenye wa polisi si wengi kama ambavyo jibu limejitokeza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, kumekuwepo na matukio mengi ya askari polisi kubambikizia wananchi kesi mbalimbali jambo ambalo limekuwa likiwavunja moyo sana wananchi kutoa ushirikiano kwa polisi, jambo hili limekuwa likijitokeza kwenye vituo mbalimbali hasa vilivyo Kata ya Isaka , Kata ya Bulige na hata Kata ya Bulyanhulu. Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atakuja kukutana na wananchi wa maeneo hayo ili kuweza kusikia kero hii na kuweza kukemea askari hao wenye tabia mbaya? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi ya maswali hayo mawili ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swalii lake la kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba siku zote tumekuwa tukihamasisha na tunaona umuhimu wa ushiriki wa wananchi katika kushirikiana na vyombo vyaa dola kukabiliana na uhalifu nchini na ndiyo maana kupitia Kamisheni yetu ya Polisi Jamii ambayo tunayo, tumekuwa tukiandaa utaratibu mzuri, ili utaratibu huo ambao umekuwa ukitumika wa kushirikisha wananchi, ikiwemo Polisi Jamii, ikiwemo Sungusungu, uweze kufuata misingi ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupitia Kamisheni yetu hii ya Polisi Jamii tumekuwa tukitoa miongozo mbalimbali,

ili wananchi waweze kutekeleza majukumu yao bila kukinzana na sheria za nchi yetu. Kama kutakuwa kuna mambo yametokea ambayo yanaweza kuwa yamesababishwa aidha na kutohana na uelewa mdogo wa ufahamu wa sheria wa jinsi ya hawa ambao wanaisaidia Polisi kutekeleza hizi shughuli za Polisi Jamii ama itakuwa mengine yametokea labda kwa makosa mengine, labda Mheshimiwa Mbunge labda atuwasilishie tuweze kuyashughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalı lake la pili kuhusiana na ubambikaji kesi, binafsi nilifanya ziara katika Mkoa wa Shinyanga na moja katika mambo ambayo niliyakemea baada ya kutembelea baadhi ya vituo na magereza katika maeneo ya Mikoa ile ya Kanda ya Ziwa na kupata malalamiko ya baadhi ya wananchi ambao walikuwa wamesema wamebambikiwa kesi, moja ni jambo hili ambalo tulilichukulia kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, ombi lake la kutaka nifanye ziara katika jimbo lak mahususi, kwa ajili ya kufanya kazi hii ambayo tumeshaifanya katika maeneo mengine ya Mkoa wa Shinyanga na mikoa mingine nchini ambayo imesaidia sana kupunguza malalamiko haya kwa wananchi tutaifanya baada ya Bunge hili kumalizika tutaandaa hiyo ziara ya kwenda jimboni kwake kwa ajili ya kushughulikia jambo hili mahususi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ungando, swalı fupi la nyongeza.

MHE. ALI S. UNGANDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Swalı langu la nyongeza. Sasa hivi Kibiti imekuwa Kibiti salama, je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha maslahi ya Polisi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba, inaboresha maslahi na mazingira ya utendaji kazi

wa vyombo vyetu vya Polisi hatua kwa hatua na kadiri ya uchumi wa nchi utakavyokuwa unaimarika.

MWENYEKITI: Tunaendelea na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Zainab Vullu.

Na. 122

Serikali Kuzuia Biashara ya Ukahaba

MHE. ZAYNAB M. VULLU (K.n.y. MHE. MAULID S. MTULIA)
aliuliza:-

Serikali inafanya juhudini kubwa ya kuzuia biashara ya ukahaba kwa kuwakamata wauzaji na wanunuzi na kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria. Pamoja na jitihada hizo bado biashara hiyo haramu inaendelea kwa kasi ileile:-

Je, Serikali ina mpango gani mbadala wa kuzuia biashara hii haramu?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikipambana na watu wanaojihusisha na vitendo vya ukahaba nchini. Jeshi la Polisi limekuwa likifanya misako kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kwa kubaini na kukamata watu ambao wanajihusisha na vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na maadili ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ukahaba ni suala mtambuka ambapo kulikabili kunahitaji ushirikiano wa wadau wengi. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kupitia Jeshi la Polisi, imeandaa mkakati wa kushirikisha taasisi

nyingine za Serikali kama vile TAMISEMI, Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii na kupunguza hatimaye kumaliza vitendo hivi ambavyo vinautia doa utamaduni wa nchi yetu. Aidha, mkakati huu unahuishisha ujenzi, kutoa elimu ya madhara ya ukahaba, faida za ujasiriamali na kuwashirikisha viongozi wa dini katika kufundisha maadili.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Zaynab Vullu.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana. Kwa kuwa, biashara mara nyingi ni muuzaji na mnunuaji; na kwa kuwa, biashara ya ukahaba mara nyingi inaita machangudoa; na kwa kuwa, katika bahari kuna changudoa, kuna changuchole, kuna changufatundu. Je, Serikali haloni kuna haja sasa ya hawa machangu wengine wakakamatwa na wakapewa elimu ya kutosha, waachane na vitendo vya ukahaba kwa sababu, wao kama hawakwenda sokoni, hii biashara haitakuwepo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha wasichana wote wanawawezesha kwa mikopo na elimu ya ujasiriamali, pamoja na juhudhi alizozisema Mheshimiwa Naibu Waziri? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, pamoja na juhudhi za Serikali, Taasisi Zisizo za Kiserikali, na baadhi ya raia kumekuwa na mkusanyiko mkubwa wa biashara hii maeneo mbalimbali, ikiwemo eneo maarufu kwa Uwanja wa Fisi, Mburahati, Dar-es-Salaam na biashara hii inafanya katikati ya maeneo wanayoishi wananchi. Je, Serikali haloni sasa kuna haja ya kwenda katika maeneo hayo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kuvunja hayo maeneo, kujenga miundombinu ambayo itawawezesha wasichana waliojiingiza katika biashara hizo kwa kutokutarajia kutokana na hali ngumu ya maisha na pia wataepukana na maradhi ya UKIMWI; Serikali ikiweza kujenga hiyo miundombinu na kuwapa mikopo hawa wasichana haioni kwamba, tutakuwa tumekwamua Taifa ambalo tunalitegemea? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, maneno mazito hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza swali lake na *concern* yake Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na janga hili. Naungana mkono na yeze kabisa kuhusiana na umuhimu wa kushughulika sio tu na wauzaji, lakini wanunuzi, lakini si tu na wanunuzi, mpaka na mazingira ambayo wale wanayaweka. Maana kuna wengine sio wanaouza, kwa mfano wenye madanguro, ni watu ambao sio wauzaji na sio wanunuzi, lakini wanahamasisha hivi vitendo. Kwa hiyo, yote hayo na wote ambao wanashiriki kwa namna moja ama nyngine katika hii biashara kuna haja ya kuhakikisha kwamba, tunachukua hatua na ndivyo ambavyo Serikali inafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo nadhani Bunge hili ni wakati muafaka wa kuzitafakari. Moja ni changamoto ya sheria; labda nitoe mfano wa sheria ambazo pengine zinakwaza mapambano dhidi ya vita ya makahaba. Ukiangalia kwenye Kanuni ya Adhabu Namba 176(a), Sura ya 16, adhabu ambayo inatakiwa itolewe kwa watu ambao wanafanya biashara ya madanguro wanasesema ni *fine* isiyozidi 500/= ama iwapo ni kosa la mara ya pili na kuendelea atatozwa *fine* isiyozidi 1,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtaona kwamba, adhabu kama hii inaweza kuwa inahamasisha utendaji wa huu uhalifu. Kwa hiyo, kuna haja ya Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuangalia na kutafakari juu ya sheria hizi ambazo zimepitwa na wakati ili hatimaye kazi kubwa ambayo inafanywa ya kuwakamata hawa makahaba kila siku, pamoja na wahamasishi wanaoshiriki na wanunuzi iweze kuwa na tija kwani mara nyngi wanapokamatwa wanarudia tena makosa kwa sababu, ya wepesi wa sheria zilizopo. Kwa hiyo, kimsingi hilo ni jibu la swali lake la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na elimu; nimhakikishie kwamba, tunaendelea kutoa elimu, lakini vilevile na mamlaka nyingine kama ambavyo nimezungumza katika swali la msingi kwamba, kwa sababu, suala hili ni mtambuka tumekuwa tunashirikiana kama Serikali na mamlaka nyingine na taasisi mbalimbali, ili kuweza kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara haya, ikiwemo kuwashirikisha vilevile viongozi wa dini ambapo nilizungumza kwamba, viongozi wa dini ni sehemu muhimu sana katika kutoa elimu ya maadili juu ya wananchi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, muda sio rafiki. Tunamalizia swali letu la mwisho, Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, sasa aulize swali lake.

Na. 123

Kukithiri kwa Vitendo vya Uhalifu

MHE. SAED A. KUBNEA aliuliza:-

Kumekuwepo na vitendo vingi vya uhalifu hapa nchini kwa watu kuvamiwa, kupigwa, kujeruhiwa na kuperwa mali zao na hata kuuawa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukomesha vitendo hivyo vya uhalifu ambavyo vinatishia usalama wa raia na mali zao?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza juhudzi za ulinzi wa raia na mali zao ili kudumisha amani na utulivu nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saed Ahmed Kubenea, Mbunge wa Ubungo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Jeshi la Polisi ina mipango mbalimbali ya kukomesha vitendo vya uhalifu kwa kuimarisha doria za miguu, pilipiki na magari, pia kufanya misako dhidi ya uhalifu na wahalifu. kutoa elimu kwa jamii kuhusu mbinu za kukabiliana na uhalifu, kufanya *operation* za mara kwa mara na kushirikisha jamii kwenye ulinzi wa maeneo yao kupitia dhana ya Polisi Jamii.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufanya juhudzi za kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao kwa kuendelea kuajiri askari na kuongeza vitendea kazi pia, kwa kutumia falsafa ya kugatua madaraka. Serikali imeshapeleka wakaguzi katika tarafa, jimbo, kata, shehiya ili kushiriki kikamilifu kwa kuyabaini maeneo tete ambayo huwa ni vyanzo vya uhalifu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri, swali langu msingi wake ni kwamba, wananchi ambao wameumizwa, wametekwa, wamepotea, sio suala la kuimarisha Vituo vya Polisi kwenye ulinzi shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa *sasa Serikali inalinda viongozi wake wakuu ardhini na angani; na kwa kuwa, sasa baadhi ya wananchi, hasa wale ambao wamekuwa na misimamo mikali ya kuikosoa Serikali, kama waandishi wa habari, wanaharakati na hasa viongozi au wanasiasa wa upinzani. [Maneno haya sio sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu je, Serikali ina mpango gani wa kushikika wa kulinda raia hawa ambao wamekuwa wakijitolea kutetea nchi yao kwa maslahi ya Watanzania wote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Serikali itakamilisha uchunguzi na kuleta ripoti Bungeni ya matukio ya kihalifu yanayofanana na ugaidi ambayo wamefanyiwa

watu mbalimbali, akiwemo Mheshimiwa Tundu Lissu, Mwandishi wa Habari wa Gazeti la Mwananchi, Abisalom Kibanda na Dokta Stephen Ulimboka na wengineo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nataka nichukue fursa hii kumpinga na kumkosoa vikali kabisa Mheshimiwa Saed Kubenea, kutokana na utangulizi wa swali lake ambalo ameuliza; na kimsingi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuititia Jeshi la Polisi, imekuwa ikihakikisha inalinda usalama wa raia wote na mali zao. Hakuna matabaka katika kusimamila ulinzi wa raia na mali zao, hiyo ndio kazi ya Jeshi la Polisi ya kila siku kwa hiyo, kusema kwamba kuna watu wanakosoa Serikali, sijui kuna watu wana nini, hizo ni kauli potofu na si sahihi na nadhani kwa mamlaka yako ungeelekeza hata zifutwe katika *Hansard*. Kwa sababu, ni upotoshwaji mkubwa kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hilo suala la kulinda usalama wa raia na mali zao jitihada kubwa zimekuwa zikifanyika. Imani yangu ni kuwa kwa kadri ambavyo tunakwenda mbele tumekuwa tukifanya hivyo kwa kutumia mbinu mbalimbali za kitaalam, kukusanya taarifa za kiintelijensia, kufanya doria, kuangalia maeneo tete, kuangalia takwimu, kumbukumbu za uhalifu nchini na ndio maana mpaka leo nchi yetu imeendelea kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoelekea katika Serikali ya Uchumi wa Viwanda, Serikali ya Uchumi wa Kati, tunaamini kabisa kutakuwa kuna mabadiliko makubwa sana ya kiteknolojia katika utekelezaji wa majukumu yake kwenye vyombo vyetu vya dola. Kwa hiyo, tutakapoimarisha na kuwekeza katika maeneo ya teknolojia tunaamini kabisa kazi hii itafanywa katika mazingira mepesi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu uchunguzi. Kazi ya uchunguzi imekuwa ikiendelea kufanyika, ingawa kazi ya uchunguzi kama alivyozungumzia yeye katika eneo mahususi la ugaidi, lina changamoto nyingi kwa sababu, tuhuma za ugaidi zinahusisha taarifa nyingine ambazo zinatoka katika mamlaka za nchi nyingine, lakini na taasisi nyingine nje ya Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, katika kufanya uchunguzi ambao unahitaji taarifa kupata katika nchi nyingine, kupata katika mamlaka nyingine, si jambo ambalo linaweza likawa limefanyika kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mpaka sasa kutokana na matukio mengi yaliyojitekeza kuna hatua kubwa imeshafikiwa katika uchunguzi wa kesi mbalimbali, ziko ambazo zimeshafika mwisho, ziko ambazo zinaendelea kuchunguzwa. Pale ambapo uchunguzi utakamilika hatua zitachukuliwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa watu wote ambao wanahusika kutoa ushirikiano kwa mamlaka katika kutekeleza majukumu yake. Mfano huu ambao ameuzungumzia wa kesi ya Mheshimiwa Tundu Lissu, tumekuwa mara nyingi tukitaka ushirikiano kutoka katika chama hiki ambacho Mheshimiwa Kubenea anatoka, ili tuweze kupata watu ambao wanaweza kutusaidia kutupa taarifa, ikiwemo dereva yule ambaye alikuwa na Mheshimiwa Tundu Lissu, lakini wenyewe wamekuwa wakifanya jitihada za kufifisha kupatikana kwa dereva huyo. Kwa hiyo, ushirikiano kwa wananchi ikiwemo na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mbunge na chama chake ni muhimu katika kukabiliana na kuharakisha uchunguzi wa kesi yetu. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu sahihi na naagiza maneno yote ya upotoshaji aliyojatao katika maswali yake ya nyongeza yafutwe kwenye *Hansard*.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza wakati wetu wa maswali na sasa ni wakati wa Matangazo. Tutaanza na

Matangazo ya Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, tunaanza na wageni walioko Jukwaa la Mheshimiwa Spika:-

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Spika, Mbunge ambaye ni *SACP Gils Muroto*, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma. Karibu sana Kamanda wetu wa Mkoa wa Dodoma katika Bunge letu. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Watapata tabu sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge kwa makofi hayo kwa Kamanda wetu.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni watano wa Mheshimiwa Joseph Kakunda, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kutoka Jimbo la Sikonge, wakiongozwa na Ndugu Thomas Juma Mayunga, ambaye ni mwanafunzi wa darasa la tano Shule ya Msingi Elimu Maalum Sikonge, mwenye ulemavu wa ngozi na bingwa wa mbio za mita 100 Kitaifa mwaka 2017/2018 kwenye mashindano maalum ya UMISHUMITA. Karibu sana mwanafunzi wetu katika Bunge letu na hongera sana kwa kazi nzuri. (*Makofi*)

Wageni sita ni wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa, Naibu Waziri wa Ujenzi, ambao ni viongozi wa Chama cha Wastaafu kutoka Kahama na Ushetu na wapiga kura wake wakiongozwa na Ndugu Wanga Mathew. Karibuni sana wageni wetu. (*Makofi*)

Wageni 17 wa Mheshimiwa Anthony Mavunde, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, (Kazi, Vijana na Ajira, ambao ni Wanakwaya wa *New Testament* ya Kanisa la Mlimwa C, wakiongozwa na Ndugu Stanford Mirambwe. Karibuni sana wanakwaya wetu. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Sonia Juma Magogo, ambao ni ndugu zake kutoka Ilala, Jijini Dar-es-Salaam. Karibuni ndugu zetu. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Venance Mwamoto, kutoka Chama Cha Wasioona Tanzania, wakiongozwa na Ndugu Clement Ndahani. Sijawaona (*Makofii*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Zaynab Bakar, ambao ni familia yake kutoka Pemba. Wale pale, karibuni sana wanafamilia wetu. (*Makofii*)

Mgeni mwingine ni wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, ambaye ni ndugu Stephen Kabindile, mdogo wake, kutoka Jijini Mwanza. Karibu sana mdogo wetu. (*Makofii*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Aeshi Hillary, ambao ni jamaa zake kutoka Mkoa wa Tanga, wakiongozwa na Mzee Jakubu Othman. Karibuni wazee wetu katika Bunge letu. (*Makofii*)

Mgeni mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Willy Qambalo, ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Dar-es-Salaam, ndugu Jaferson Makere. Karibu, yuko pale juu. (*Makofii*)

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Amina Makilagi, ambaye ni Afisa Mtendaji wa Kata ya Mwigobero, Musoma, Mkoani Mara, Ndugu Mfungo Bunini. (*Makofii*)

Wageni wengine ni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wajumbe 30 wa Baraza la Wazazi la Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Kimara, Jijini Dar-es-Salaam. Karibuni Wajumbe wetu wa Baraza la Wazazi. (*Makofii*)

Pia kuna wanafunzi 100 na Walimu nane kutoka shule ya Jumapili ya kanisa la Moravian, Jimbo la Kaskazini Dodoma. Karibuni sana wanafunzi wetu. (*Makofii*)

Vile vile wapo wanafunzi 84 na Walimu 10 kutoka Shule ya *Green View English Medium Primary School* ya Jijini Mwanza wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wao, Mwalimu Kennedy Joshua. Karibuni sana wanafunzi wetu kwa ajili ya mafunzo katika Bunge letu. (*Makofii*)

Wapo pia wageni sita kutoka Kisasa, Jijini Dodoma, ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendeshwa, wakiongozwa na ndugu Glory Shayo. Karibuni sana kwa ajili ya mafunzo yenu. (*Makof*)

Mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi ambaye ni Spika wa Bunge la Wanachuo cha Ardhi, ndugu Kamara Muberwa. Karibu sana Spika la Bunge la Wanachuo. (*Makof*)

Wengine ni Wakazi tisa (9) wa Mkoa wa Arusha ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Wakazi tisa wako pale, karibuni sana kwa ajili ya mafunzo. (*Makof*)

Wanafunzi wawili (2) kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosomea Sheria mwaka wa nne (4). Karibuni sana wanafunzi wetu. (*Makof*)

Tangazo lingine ni tangazo la Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba Wizara ya Maliasili na Utalii imeandaa Tamasha la Urithi ili kuenzi utamaduni na urithi wa Mtanzania. Tamasha hili linaitwa Urithi *Festival cerebrating our Heritage* na litakuwa linafanyika mwezi Septemba kwa kila mwaka kuanzia mwaka huu 2018. Dhumuni la Tamasha ni kuenzi na kunadi kiutalii hazina kubwa ya utamaduni mila na desturi za makabilা yote nchini, ambayo ni zaidi ya 128. Tamasha litasherehekewa mwezi mzima wa Septemba.

Uzinduzi rasmi utakuwa kesho tarehe 15 Septemba, 2018 katika uwanja wa Jamhuri ambapo Mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, Mheshimiwa Spika anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kushiriki katika uzinduzi huo. Aidha, Waheshimiwa Wabunge na Mawaziri wote watakaokuwepo kesho wanaombwa kujumuika na Mgeni Rasmi saa 3.00 asubuhi katika kuadhimisha siku hii muhimu kwa Taifa letu. Pia wote mnahamasishwa kuвая nguо za

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

asili na utamaduni katika siku hiyo ya uzinduzi ili kutoa hamasha kwa wananchi kuthamini mavazi ya asili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kukamilisha matangazo hayo, sasa namkaribisha Mheshimiwa Spika aweze kuendelea na shughuli zilizobaki. (*Makofi*)

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti

SPIKA: Katibu.

KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mwongozo wa Spika.

SPIKA: Katibu.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mwongozo wa Spika.

KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli za Mkutano wa 12 wa Bunge sasa zimemalizika.

SPIKA: Katibu.

KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Hoja ya kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. (*Makofi*)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, leo hii tunafikia tamati ya Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge lako Tukufu ambao ulianza likao chake cha kwanza tarehe 4 Septemba, 2018. Hivyo hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwiningi wa rehema kwa kutuwezesha kuhitimisha shughuli zote zilizopangwa kwenye Mkutano huu tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Spika, vile vile nashukuru sana na nikushukuru wewe binafsi kwa umahiri wako mkubwa wa kuliongoza Bunge hili Tukufu, ukisaidiwa na Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango mizuri mliyoitoa kwa kusema na kwa maandishi wakati wa mijadala ya hoja mbalimbali zilizowasilishwa na Serikali kwenye Mkutano huu. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wenzangu kuwa Serikali imepokea michango yenu ambayo inaamini itasaidia sana kuboresha utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kukupa pole kufuatia taarifa za kuhuzunisha za kifo cha Mheshimiwa Stephen Hillary Ngonyani, aliyekuwa Mbunge wa Korogwe Vijiji kilichotokea tarehe 2 Julai, 2018. Aidha, natoa pole kwa familia ya marehemu na wananchi wote wa Korogwe Vijiji kwa kumpoteza mwakilishi wao. Vile vile katika kipindi hiki wapo baadhi ya Wabunge wenzetu ambao wamepoteza wapendwa wao. Kipekee natoa salaam za pole kwa Mheshimiwa Joseph Leonard Haule maarufu Profesa J., Mbunge wa Mikumi na Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi maarufu Mr. Sugu, Mbunge wa Mbeya Mjini kwa kuondokewa na wazazi wao. Kadhalika niungane na Bunge zima kumpa pole Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kufiwa na dada yake Bi. Monica Joseph Magufuli. Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kuwapa pole Watanzania wenzangu waliopoteza ndugu, jamaa na

marafiki na wengine kupata ulemavu katika matukio mbalimbali ya ajali za barabarani; wakiwemo watalii wane (4) kutoka nchi za Hispania na Italia waliofariki dunia baada ya gari lao la utalii kugongana na lori Wilayani Monduli. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi na awape nafuu majeruhi wote wapone haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo hilo kufuatia uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni. Ushindi huu ni ishara ya imani kubwa walionayo wananchi wa Jimbo la Buyungu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa mkutano huu Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kuuliza maswali ya msingi yapatayo 123 na maswali ya nyongeza 380 ambayo yalijibowi na Serikali. Vile vile Serikali ilitoa kauli kuhusu hali ya sukari nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujadili Miswada mitano (5) iliyowasilishwa na Serikali katika Mkutano huu. Aidha, Bunge lako Tukufu lilipokea na kupitisha Taarifa ya Kudumu ya Bunge ya Sheria ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Miswada ya sheria iliyojadiliwa na kupitiwa na Bunge lako Tukufu katika mkutano huu ni kama ifuatavyo:-

(1) Muswada wa Sheria kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi wa Mwaka 2018 (*The Dodoma Capital City (Declaration) Bill, 2018*);

(2) Muswada wa Sheria wa Bodi ya Kitaalam ya Walimu Tanzania wa mwaka 2018 (*The Teachers Professional Board Bill, 2018*);

(3) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na.2 wa mwaka 2018 (*The Written Law (Miscellaneous Amendments) No.2 Bill, 2018*);

(4) Muswada wa Sheria za Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.3 wa mwaka 2018 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.3 Bill, 2018*); na

(5) Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya Mwaka 2018 (*The Public Private Partnership (Amendments) Bill 2018*).

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri iliyotolewa wakati wa kujadili Miswada hiyo muhimu yenye manufaa mingi kwa nchi yetu. Serikali itafanyia kazi maoni na ushauri ilitotolewa kwa lengo la kuhakikisha kwamba utekelezaji wake unawanufaisha wananchi nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri ya kuwasilisha Miswada ilijojadiliwa katika Mkutano huu pamoja na kutoa ufanuzi mbalimbali wakati wa kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Aidha, nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalam wake kwa kazi nzuri ya kuandaa Miswada iliyowasilishwa katika Mkutano huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nipitie maeneo ya msisitizo kisekta. Kabla ya kuhitimisha Mkutano huu naomba nieleze masuala yafuatayo ili kuweka msisitizo kwa viongozi, watendaji na wananchi kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yao ya kuwaletaa maendeleo wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasimamia ipasavyo utekelezaji wa bajeti sambamba na kuongeza uwajibikaji na nidhamu ya matumizi ya fedha zilizolekezwa katika vipaumbele mbalimbali kama ilivyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali kadhalika Serikali inaendelea kuimarisha ukaguzi

katika ngazi zote na ufuutiliaji wa karibu wa miradi ya maendeleo na kufanya tathimini ya mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba miradi na kazi vina uwiano na thamani ya fedha za umma zinazotolewa kwa Serikali kwa lugha nyingine *value for money*.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019, Serikali inashirikiana na sekta binafsi, wadau wa maendeleo na wananchi wote ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Serikali iliwasilisha Bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Kat i ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2018 (*The Public Private Partnership (Amendment) Bill, 2018*). Marekebisho hayo ya Sheria yanalenga kuimarisha mfumo wa kitaasisi na kisheria katika kusimamia miradi ya ubia. Vilevile, kutatua changamoto zilizopo katika miradi ya PPP ili kurahisisha ubuaiji, uidhinishaji na utekelezaji wake sambamba na kuchoecha haraka maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ameweka dhamira ya dhati ya kufanya kazi kwa juhud i na maarifa ili kutimiza ndoto na matarajio ya Watanzania ya kujenga nchi yenye uchumi imara. Katika kipindi hiki, tumeshuhudia mambo makubwa aliyoafanya yakiwemo kujenga ari ya uzalendo kwa kuilinda na kuisemea nchi yetu bila woga; kudumisha amani, utulivu na mshikamano; kuimarisha ulinzi na usalama; kudhibiti na kupambana na dawa za kulevy a.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila iwapo sitotaja japo kwa uchache hatua mbalimbali tena za makusudi zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Rais katika kuwalet ea maendeleo Watanzania na kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, wenzetu Wachina wanao msemo usemao "*Empty Talk, Harm the Country*" ambao kwa tafsiri isiyo rasmi ya Kiswahili unamaanisha "Porojo, hudhuru Nchi". Msemo huo uliotumika sana kipindi Uchina inaingia katika

maboresho ya kiuchumi miaka ya 70 na 80 chini ya Kiongozi wa kipindi hicho mwana mageuzi *Deng Xiaoping*, ulilenga kuhamasisha uchapa kazi kama ilivyo sasa falsafa ya Serikali ya Awamu ya Tano ya "Hapa Kazi Tu". (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kinachokaribia miaka mitatu sasa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amedhihirisha si tu kwa uzalendo wake kwa Taifa lakini pia katika kusimamia mipango ya maendeleo lakini pia kulinda rasilimali za Taifa kwa lengo la kuwanufaisha Watanzania wa kizazi kilichopo na kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mchango wa Mheshimiwa Rais, naomba nitaje baadhi ya maeneo ambayo yanaakisi moja kwa moja juhudii zake hizo:-

- (1) Kujenga ari ya kufanya kazi;
- (2) Kuimarisha nidhamu, uadilifu na uwajibikaji ndani ya utumishi wa umma na kukemea uzembe;
- (3) Kuendesha vita dhidi ya rushwa na ujisadi kwenye taasisi za umma sambamba na kuanzisha Mahakama ya Mafisadi;
- (4) Kuimarisha ulinzi wa rasilimali za nchi ikiwemo madini na maliasili;
- (5) Kufufua Shirika la Ndege la Tanzania ili kuimarisha usafiri wa anga na kukuza sekta mtambuka zikiwemo utalii, afya na kilimo;
- (6) Kujenga reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa (*SGR*);
- (7) Kuendeleza ujenzi wa barabara zikiwemo barabara za juu (*flyovers*);

(8) Kununua meli (Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria) na kuweka vivuko vipyta (Lindi-Kitunda, Kigongo Ferry, Ukerewe na kadhalika);

(9) Kujenga vyanzo vipyta vya umeme kama vile mradi wa kuzalisha umeme wa maji megawati 2,100 katika bonde la Mto Rufiji;

(10) Kusambaza umeme hadi vijijini sanjari na kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu ya mpango wa REA ili kufikia lengo lililokusudiwa;

(11) Kutekeleza mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga hapa kwetu Tanzania;

(12) Kuimarishe huduma za afya hususan upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaatiba katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya pamoja na ujenzi wa Vituo vya Afya na Hospitali za Wilaya;

(13) Kutoa Elimumsingi Bila Malipo kwa watoto wa Kitanzania;

(14) Kuhakikisha miradi yote ya maji inayotekelizwa inakuwa bora, yenye uwiano na thamani halisi ya fedha pamoja na kukamilishwa kwa wakati; na

(15) Kuimarishe kilimo, ushirika na bei za mazao ya biashara.

Mheshimiwa Spika, juhudii zote hizo zinafanywa kwa lengo la kuiwezesha nchi yetu kufikia malengo ya dira ya Taifa ya kuwa na uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo mwaka 2025. Niwaombe Watanzania wenzangu tuendelee kuunga mkono juhudii za Mheshimiwa Rais katika kuleta maendeleo. Kadhalika, nitoe wito kwa wawekezaji kutumia fursa ya uwepo wa mazingira mazuri nchini ya uwekezaji, biashara na upatikanaji wa malighafi wa kujenga

viwanda mbalimbali hususan vya kuchakata mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo; Hali ya Chakula Nchini; hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula na upatikanaji wake hapa nchini imeendelea kuimarka. Tathmini iliyo fanyika mwezi Juni, 2018 inaonesha kwamba uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2017/2018, ni tani milioni 16.9. Kati ya hizo tani milioni 9.5 ni mazao ya nafaka na tani milioni 7.4 ni mazao yasiyo ya nafaka. Kutokana na uzalishaji huo na kwa kuzingatia mahitaji ya chakula nchini ambayo ni tani milioni 13.6, kutakuwa na ziada ya tani milioni 3.3. Hivyo, nchi itajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 124.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Serikali inaendelea kuwasihii wananchi kutumia akiba hiyo ya chakula kwa uangallifu kwani zipo nchi jirani ambazo zina uhaba mkubwa wa chakula. Vilevile, naziagiza taasisi zote zinazosimamia elimu ya lishe na afya kuongeza nguvu zaidi ili kupunguza kiwango cha udumavu na utapiamlo hususan kwa watoto wadogo kwenye maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo; Serikali inaendelea kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa pembejeo muhimu za kilimo kwa wakati. Katika msimu wa kilimo 2018/2019 hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Agosti, 2018, upatikanaji wa mbolea aina zote umefikia kiasi cha tani 215,207 na matarajio kwa msimu huu wa 2018/2019 ni kutumia tani 485,000. Vilevile, Serikali imewe ka mikakati thabiti ya upatikanaji wa mbegu bora kwa mazao ya kipaumbele. Wakala wa Mbegu wa Serikali (ASA) umepanga kuzalisha na kusambaza tani 40,000 na sekta binafsi na inatarajia pia kuingiza tani 20,645 za mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani sana kwa Taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation* kwa kukubali kushirikiana na Serikali kuboresha mfumo wa Taifa wa upatikanaji wa mbegu bora nchini. Mfumo huo utahusisha uboreshaji wa uzalishaji wa mbegu mama katika vituo vya utafiti; kuimarisha na kuboresha miundombinu ya mashamba ya

Wakala wa Mbegu wa Serikali (*ASA*); na kujenga uwezo wa Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (*TOSCI*); na kuboresha mfumo wa menejimenti ya upatikanaji, usambazaji na matumizi ya mbegu bora nchini.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo msimu wa kilimo unaanza miezi michache ijayo, Serikali itahakikisha upatikanaji na matumizi sahihi ya viuatilifu kwa mazao mbalimbali. Mathalan, Serikali itawezesha upatikanaji na matumizi ya ekapaki milioni saba za viuatilifu vya zao la pamba kwa mwaka 2018/2019. Aidha, Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 10 katika msimu wa mwaka 2018/2019, kwa ajili ya kupambana na wanyama na wadudu waharibifu kama vile *quelea quelea*, viwavijeshi na panya pamoja na visumbufu vingine vya mazao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliamua kurejesha ununuzi wa mazao hayo makuu ya biashara kupitia vyama vya ushirika kwa lengo la kuwanufaisha wakulima. Katika kufanikisha azma hiyo, Serikali inasimamia matumizi ya mifumo mbalimbali ya masoko ikiwemo Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa (*Commodity Exchange*). Matumizi ya mifumo hiyo yamechangia kuboresha ununuzi wa mazao hayo. Kwa mfano, biashara ya mazao hayo ambayo imekuwa ikifanywa kwa njia za mnada na kusimamiwa na Vyama vya Ushirika imeleta chachu ya ushindani na hivyo kumpatia tija mkulima.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la pamba hadi kufikia Agosti 2018, kilo milioni 226 za pyenye thamani ya Shilingi bilioni 248.6 zilikusanywa. Aidha, Vyama vya Ushirika vimeendelea kusimamia ubora wa pamba katika msimu wa 2018/2019 ambao umeongezeka maradufu ikilinganishwa na msimu wa 2017/2018. Kwa mfano, msimu wa 2018/2019, pamba ya daraja la kwanza ilikuwa asilimia 44.2 ikilinganishwa na asilimia 22.7 ya msimu wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika zao la korosho, mfumo wa ununuzi kupitia Vyama vya Ushirika unapata mwitikio mzuri kutoka kwa wakulima na wanunuzi. Hali hiyo, imesaидia

wakulima kupata bei za ushindani ambapo kwa msimu 2017/2018, ilifika Sh.4,100 kwa kilo ikilinganishwa na Sh.2,700 ya msimu wa 2016/2017. Aidha, uzalishaji umeongezeka ambapo jumla ya tani 296,281 za korosho ghafi zenyet thamani ya shilingi takribani trillioni 1.12 zilikusanywa na kuuzwa kuitia Vyama vya Ushirika ikilinganishwa na tani 265,000 kwa msimu uliopita.

Mheshimiwa Spika, zao la kahawa, kwa msimu huu wa 2018 uzalishaji wake unakadiriwa kuwa tani 65,000 ikilinganishwa na tani 42,513 za msimu wa 2017/2018. Hadi sasa, tani 14,664 zimeshauzwa kuitia Vyama vya Ushirika 643 na kuingiza Dola za Marekani elfu 24.4 Serikali inaendelea kusimamia mwenendo wa masoko ya kahawa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la tumbaku hadi kufikia Agosti 2018, wakulima wamekusanya na kuuza tumbaku kiasi cha kilo millioni 33.1 zenyet thamani ya shilingi bilioni 119.5 kuitia Vyama vya Ushirika. Hadi sasa tunaendelea kukabiliana na changamoto zinazokabili zao hili la tumbaku ikiwemo na masoko.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa zao la chai, hadi kufikia Agosti 2018, kiasi cha tani 31,814 za majani mabichi ya chai zenyet thamani ya shilingi bilioni 9.9 kimekusanywa na kuuzwa kuitia Vyama vya Ushirika katika Mikoa ya Njombe, Iringa, Tanga na Mbeya. Serikali inaendelea kuimarisha ununuzi wa majani mabichi ya chai maeneo yote kwenye mikoa inayozalisha.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula; sambamba na azma ya Serikali ya kuweka mkazo katika kusimamia uzalishaji na masoko ya mazao makuu matano ya biashara ambayo ni pamba, kahawa, korosho, chai na tumbaku, Serikali pia, imedhamiria kupanua wigo kwenye mazao mengine muhimu ikiwemo zao la chikichi, alizeti na ufuta ili kukidhi uzalishaji wa mbegu za mafuta hapa nchini. Katika kutekeleza azma ya Serikali kuhusu kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini, tarehe 28 Agosti, 2018 nikiwa Mkoani Kigoma nilizindua kampeni maalum ya

kuendeleza zao la chikichi ambalo kwa sasa linatambulika kama zao kuu la sita la kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, malengo ya kampeni hiyo ni kuhakikisha kuwa Mkoani wa Kigoma na maeneo mengine yenye fursa ya kulima zao la chikichi yanaimarisha kilimo hicho. Hatua hiyo, inakusudia kuiwezesha Tanzania kuachana na uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje baada ya muda mfupi. Hivi sasa, nchi yetu inatumia takribani Dola za Marekani milioni 294 kila mwaka kwa ajili ya kuagiza mafuta hayo. Kampeni hiyo inaendelea katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba tunajitosheleza kwa mahitaji ya mafuta ya kula, Serikali imeweka mikakati ya kuendeleza zao la chikichi kama ifuatavyo:-

(1) Tumeanzisha Kituo cha Utafiti wa zao la chikichi mkoani Kigoma kwenye eneo la Kihinga;

(2) Kuandaa Mpango Mkakati wa uzalishaji wa miche bora ya chikichi milioni 20 ifikapo mwaka 2021. Kwa kuanzia, Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali inakusudia kuzalisha miche bora ya chikichi milioni 10 na kusambazwa kwa wananchi wenye nia ya kulima chikichi;

(3) Kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa utafiti wa mbegu bora ili kuongeza tija kutoka tani 1.6 hadi kufikia tani nne(4) za matunda ya chikichi kwa heka kwa mwaka;

(4) Kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa ajili ya uchakataji wa zao la chikichi; na

(5) Kusimamia vituo vikuu vya uzalishaji vya Gereza la Kwitanga na llagala na JKT Bulombora yaliyoko Mkoani Kigoma na tumetenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje wanaohitaji kuwekeza kwenye zao la chikikichi.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wananchi kuchangamkia fursa ya kilimo cha zao la chikichi ili tuweze kujitosheleza kwa mafuta ya kula na ziada kuweza kuuza nje. Vilevile, nitoe rai kwa wawekezaji kuanzisha viwanda vyta kuchakata chikichi na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, Upimaji wa hiari wa VVU; itakumbukwa kuwa tarehe 19 Juni, 2018, Jijini Dodoma, nilizindua kampeni ya Kitaifa ya kupima kwa hiari VVU pamoja na kuanza mapema matumizi ya dawa za kufubaza (ARV) kwa wale watakaogundulika kuwa na maambukizo. Kampeni hiyo, ijlukanayo kama "FURAHA YANGU, PIMA, JITAMBUE, ISHI" iliwalenga Watanzania wote kujitokeza kupima na kutambua afya zao hususan wanaume ambao hawajitokezi kwa wingi kupima na kutambua afya zao. Wanaume wengi tumekuwa tukitumia wenza wetu katika kutambua kama tumeathirika au la. Tunakaa majumbani tunasubiri tu, ukimwona mwenza wako anarejea kutoka kliniki na furaha na wewe unajipa matumaini kuwa umesalimika. Sasa wanaume wenzangu tubadilike, tuanze kuchukua hatua za kupima na kutambua afya zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikiwa kinara wa kampeni hiyo, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Septemba, 2018 tayari mikoa 14 imeanza kutekeleza Kampeni hiyo. Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kigoma, Manyara, Mbeya, Mtwara, Mwanza, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Tabora na Tanga. Niwapongeze Wakuu wa Mikoa hiyo kwa kutekeleza jukumu lao na niwatake waendelee kuhimiza wananchi waliopo kwenye maeneo yao hususan wanaume kutambua afya zao kuhusu maambukizo ya VVU kuititia kampeni hii.

Mheshimiwa Spika, niwatake Wakuu wa Mikoa ambayo bado haijaanza kutekeleza Kampeni hiyo kuanza mara moja. Kwa kutambua umuhimu wa Kampeni hii, ifikapo Desemba Mosi, 2018 wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani tutafanya tathmini ya utekelezaji kwa mikoa yote nchini. Kwa msingi huo, nisisitize

wadau wote wenye mapenzi mema na nchi hii wasaidie kutekelezaji kampeni hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, Serikali inafanya juhudzi za kufikisha kampeni hii katika Ligi kuu ya Mpira wa Miguu Tanzania Bara kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (*TFF*). Tunafanya hivyo kwa kutambua kuwa Mpira wa Miguu ni mchezo unaoongoza kwa kupendwa duniani na Tanzania. Aidha, kufuatia hatua ya Kituo cha matangazo ya Televisheni cha Azam kuamua kuonesha ligi yetu, watu wengi wamepata mwamko wa kutazama na kufuatilia michezo ya Ligi kuu Tanzania. Hivyo, tuna uhakika wa kuwafikia wananchi wengi na kuwahamasisha kuchukua hatua za kupima VVU na wale watakaogundulika kuwa na maambukizi kuanza mapema matumizi ya *ARV*.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kukupongeza wewe mwenyewe binafsi kwa kuonesha mfano, pia kwa kupima na kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako Tukufu kupima na kutambua afya zao. Kwa hiyo, tunaamini kampeni hii pia itabebwa na Waheshimiwa Wabunge wote ili iweze kuenezwa nchini kote.

Mheshimiwa Spika, Uagizaji wa Mafuta ya Kula na Sukari; katika Mkutano huu ulijitokeza mjadala kuhusu suala la usimamizi na uangalizi wa mafuta ya kula na sukari. Serikali kwa upande wake inaimarisha taratibu za uingizaji wa sukari na mafuta ya kula kwa kuweka madaraja na usimamizi makini. Aidha, naagiza Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kukamilisha jukumu hilo kwa wakati. Pia, nategemea vyombo vy ya Dola kuongeza ushirikiano na mamlaka husika (*TRA, TFDA*, Bodi ya Sukari na *TBS*) kudhibiti uingizaji holela wa sukari na mafuta ya kula ikiwa ni pamoja na kuziba mianya ya magendo.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Michezo; katika nyanja ya michezo naomba nitoe pongezi za dhati kwa Timu ya Taifa ya Wanawake (*Kilimanjaro Queens*) kwa kutwaa kombe la Afrika Mashariki. Vilevile, nawapongeza vijana wetu wa

umri chini ya miaka 17 (*Serengeti Boys*) kwa kuwa washindi wa tatu kwa ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwenye mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF). Pia nimpongeze Mwanamasumbwi wa Kitanzania Hassan Mwakinyo kwa kumchapa Bondia Mwingereza Sam Egginton kwenye raundi ya pili ya pambano lao la masumbwi lililofanyika huko Birmingham, Uingereza. Hongereni sana wanamichezo wetu na endelezeni moyo huo wa kizalendo mliouunesha katika kulitangaza Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019 Tanzania itakuwa mwenyeji wa mashindano ya mpira wa miguu kwa vijana chini ya umri wa miaka 17 (*AFCON-Under 17*) yanayoandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika. Hii ni fursa nyingine ya kipekee ya kulitangaza Taifa letu katika nyanja za Kimataifa. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na maandalizi stahiki ambayo yatahusisha ukarabati wa viwanja vitakavyotumika katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa wananchi watumie vizuri uwepo wa mashindano hayo kujijengea kipato hususan kupitia biashara ya bidhaa na huduma kwa wageni. Vilevile, natoa wito kwa Watanzania wote kuwa wazalendo kwa kuunga mkono timu zetu zinazoshiriki mashindano ya kimataifa ili zipate mafanikio.

Mheshimiwa Spika, wakati nikielekea kuhitimisha hotuba yangu hii kuna masuala ambayo ningependa kuyasisitiza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kudumisha Amani; ni vema tukatambua kwamba vita ya kiuchumi aliyoitangaza Mheshimiwa Rais, mafanikio yake yatategemea kwa kiasi kikubwa uwepo wa amani, umoja na mshikamano wa Kitaifa. Tarehe 22 Oktoba 1987, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere akiwa Mjini Dodoma aliwahi kusema na naomba nimnukuu:

"Tuna haki ya kujivunia umoja huu na amani hii, maana ndivyo vilivyotuwezesha kupambana na matatizo makubwa ya vita ya uchumi, na hata ya kisiasa". Mwisho wa kunukuu. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nimenukuu maelezo hayo ya Mheshimiwa Rais wa Kwanza wa Tanzania ili kuwakumbusha Watanzania wenzangu kwamba amani tulyonayo ni muhimu katika kufikia malengo yetu ya kiuchumi. Hivyo, tuidumishe, tuithamini na tuilinde amani tulyonayo.

Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya msimu wa kilimo; kuanzia mwezi Septemba, 2018 maeneo mbalimbali ya nchi yetu yameanza kupata mvua za vuli ambazo huashiria kuanza kwa msimu mpya wa kilimo. Serikali inahakikisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea na viuatilifu kwa ajili ya msimu huu mpya wa kilimo unawezeshwa. Hivyo, nitumie fursa hii kuwashimiza mawakala na wafanyabiashara walipewa jukumu la kusambaza pembejeo kuhakikisha kuwa zinawafikia wakulima kwa wakati. Aidha, niwasih i wakulima kuandaa mashamba yao mapema ili waweze kutumia vizuri mvua za vuli ambazo zinaanza kunyesha katika baadhi ya maeneo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kuimarisha na kusimamia Ushirika; katika kipindi kifupi Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kurejesha imani ya wananchi kuhusu ushirika. Aidha, katika kipindi hicho wananchi wameendelea kuona na kunufaika na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kusimamia sekta ya ushirika.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaendelea kujenga ushirika imara sanjari na kuhakikisha kwamba wakulima wananaufaika na usimamizi mzuri wa vyama vyaya Ushirika. Hivyo, naendelea kuwasisitiza viongozi wenye dhamana katika kusimamia ushirika nchini kuhakikisha wanachukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo dhidi ya watakaothubutu kuhujumu ushirika.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe hotuba yangu kwa kumshukuru Katibu wa Bunge na watendaji wa Ofisi ya Bunge kwa kazi kubwa ya kuratibu vikao vya Mkutano huu. Aidha, niwashukuru watendaji wa Serikali kwa kufanikisha shughuli zilizopangwa na Bunge lako Tukufu kwa weledi na ufanisi mkubwa. Kipekee, niwashukuru wanahabari wote kwa kufikisha habari kuhusu Mkutano huu kwa wananchi. Nivishukuru pia vyombo vya ulinzi na usalama kwa huduma wanazozitoa kwa washiriki wa Bunge hili bila kuwasahau madereva waliohudumia wakati wote tukiwa hapa Bungeni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwatakia safari njema Waheshimiwa Wabunge, niwaombe wanaporejea majimboni kwao kuwaeleza wananchi mambo yaliyojiri hapa Bungeni. Wapeni taarifa wananchi juu ya matarajio yetu kwao na kuwasahi waendelee kutuunga mkono kwenye jitihada zetu katika kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 14 Novemba, 2018 siku ya Jumanne, saa tatu kamili asubuhi litakapokutana tena katika ukumbi huu Jijini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono kweli kweli. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yako nzuri, ahsante sana. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa hoja ya kuahirisha Bunge Wajibu wangu ni kuwahoji. (*Makofii*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

SPIKA: Basi Waheshimiwa Wabunge, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli kwa mara nyingine kwa hotuba yake, pamoja na mambo mengine aliyoyazungumzia amemtaja Bondia Hassan Mwakinyo ambaye amefanya jambo kubwa sana la kutuletea heshima kubwa katika nchi yetu.

Sasa Waheshimiwa Wabunge kwa heshima kubwa naomba nimlete kwenu bondia Hassan Mwakinyo, pale ulipo naomba usimame. (*Makofi/Vigelegele*)

Hapo, hapo tu. Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, ndugu yetu Hassan Mwakinyo tunakupongeza sana, tuna fahari kubwa sana kwamba wewe ni mwenzetu na umeliletea taifa letu heshima kubwa sana na ni matarajio yetu kwamba bado utasonga mbele na kupata mataji makubwa zaidi kuliko hata hapo. (*Makofi*)

Tutakapomaliza kuahirisha kila kitu hapa nitaomba Wasaidizi mtamchukua Hassan Mwakinyo aende ampe mkono Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwepo popote pale. (*Makofi*)

Ahsante sana, naomba ukae, karibu sana.

Tunawapongeza Wabunge wa Tanga. Mimi sikujua kama Tanga inaweza ikatoa Bondia. Nilijua bondia anaweza kutoka Usukumanii hivi, kwa Wanyamwezi hivi wabeba mizigo mizito, lakin kumbe ndiyo hamna chochote huko. (*Makofi/Vicheko*)

Ndiyo Mheshimiwa Aeshi.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. KHALFAN H. AESHI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nataka kuomba mwongozo wako, tumekuwa tukiwachangia sana Ma-Miss humu ndani leo hii tunaomba Mheshimiwa Mwongozo wako sisi Wabunge *at least* tuweze kumchangia hata Sh.20,000/= kila mmoja

kwa sababu tumekuwa tukichanga sana. Mheshimiwa naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

SPIKA: Kwa makofi haya limeafikiwa si ndio eeeh?

WABUNGE: Ndiyooo.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, Sh.20,000/= ni ndogo.

SPIKA: Tumeshahoji ni Sh.20,000/=. Ahsante sana.

(Bunge liliridhia kila Mbunge kukatwa Sh.20,000 ikiwa ni pongezi kwa Bondia Hassan Mwakinyo)

SPIKA: Pia naomba niwatambulise Wabunge wawili (2) ambao safari hii walienda kwene Ibadha ya Hija na wamerudi salama na sasa Wabunge hawa ni Maalhaj. Kwanza ni Mheshimiwa Mussa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto. Sasa yeze rasmi ni Mheshimiwa Alhaj Mussa Shekilindi; na wa pili ni Mbunge wa Bagamoyo Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, sasa ni Alhaj Shukuru Kawambwa. (*Makofi*)

Ahsante sana.

WABUNGE FULANI: Umemsahau Masauni.

SPIKA: Alienda pia? Oooh!

WABUNGE FULANI: Eeeh. (*Makofi/Vicheko*)

SPIKA: Samahani Waheshimiwa naambiwa pia *Engineer* Masauni ameenda Hija safari hii. Kwa hiyo tunaye Alhaj mwingine Mheshimiwa Masauni. (*Makofi/Vicheko*)

WABUNGE FULANI: Sheikh Nassir.

SPIKA: Na Sheikh Nassir eeeh? Jamani ameongezeka na mwingine Sheikh Nassir. (*Makofi*)

Ahsante sana. Sasa tumewataja jamani pamoja na mambo mengine, wale wenzangu mimi wenyewe vijicho pembe aaah sasa hawa Maalhaj jamani. (*Makofi/Vicheko*)

Waheshimiwa Wabunge jana niliwaambia kwamba nitafanya zoezi kidogo la takwimu ya kuona Bunge letu likoje kiusomi. Sasa nimefanya kidogo *homework* yangu lakini nitataja takwimu chache tu. Takwimu zangu zinaniambia kwanza upande wa umri Mbunge kijana kuliko wote ni Mheshimiwa Halima Bulembo ana miaka 27 na Mbunge mwenye umri mkubwa kuliko wote ana miaka 75, kwa leo hayupo hapa. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa ujumla ilikuwa baadhi ya watu wanapenda kuliita Bunge hili ni Bunge la vijana, lakini niwaambie baada ya takwimu zangu hizi, Wabunge wenyewe umri wa miaka 40 na kwenda mbele ni asilimia 80 ya Wabunge wote. Kwa hiyo, haya maneno ya kusema Bunge la Vijana siyo kweli. Unajua ujana wakati mwingine ni *attitudinal*, mtu anafikiri bado kumbe umri umeshakwenda. (*Makofi/Kicheko*)

Sasa upande wa elimu nianze na kundi maalum la Viti Maalum. Kwanza kwenye elimu huku nimeangalia elimu ya sekondari na kwenda mbele, hawa wa elimu ya msingi sikuweza kuwaangalia vizuri, kwa hiyo takwimu hiyo nitaiacha mpaka siku nyingine.

Elimu ya sekondari kwa Viti Maalum wote wenyewe elimu ya sekondari ni 24. Katika hao 24 *CUF*watano (5), CHADEMA watano (5) na CCM 14. Wenyewe *Certificate* na *Diploma CUF* wane (4), CHADEMA nane (8) na CCM 16. Wenyewe *Bachelor* na kuendelea *CUF* mmoja (1), CHADEMA 23 na CCM 32. Katika Viti Maalum upande wa Shahada ya Uzamivu (*PhD*) ni 11 kwa ujumla wake; 10 CCM na CHADEMA mmoja (1). Hizi takwimu zinasaidia kuonesha wale wanopendaga kusema ooh ooh, kumbe siyo kweli bwana, bado CCM inatamba. (*Makofi*)

Basi na uchambuzi mwingine bado unaendelea. Kwa kweli, Maprofesa tunao saba (7) na wote saba (7) ni wa CCM.

PhD kwa nyumba nzima hii ziko 29; mmoja (1) *CUF*, mmoja (1) CHADEMA na 27 CCM. Maana yake watu kwenye mitandao wanasema ooh CCM imejaza vihiyo, sasa takwimu hizo. Kwa ujumla wake wapo baadhi huwa wanasema Bunge hili ndiyo Bunge ambalo tangu historia hajjawahi kutokea Bunge la namna hii. Kwa aina hii ya elimu niliyioieleza hili ni Bunge la Kumi na Moja toka tupate uhuru, hakuna Bunge limewahi kuwa na wasomi wengi kuzidi hili Bunge la Kumi na Moja. Huo ndiyo ukweli wenyewe na ndiyo hali halisi. (*Makofi*)

Nilikuwa naangalia kule Buyungu kwa Mheshimiwa Chiza walipogombea wale wa CCM walikuwa kama 22 (*around that number*). Wale wagombea waligombea kwa CCM peke yake wote 22 ni ma-*graduate*, Buyungu. Yaani hiyo inakupa picha ya mabadiliko ya nchi sasa na inapoelekea, yaani kama Buyungu hali ni hiyo basi kwa vyovoyote vile na kwingine nako kutakuwa kumechangamka kwa namna hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo niliyoyatoa, sasa naomba tusimame ili tusikilize Wimbo wa Taifa, *Brass Band* mnawenza mkaendelea sasa.

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

SPIKA: Ahsante sana, mnawenza mkakaa. Kwenye takwimu zangu takwimu moja muhimu sikusema ni kwamba wale wenye *1st Degree* na *Masters* ujumla wake humu ndani ni 161, ni nyingi sana hizi. Katika hizo *CUF* wanazo 14, CHADEMA wana 31 na CCM wanazo 114. (*Makofi*)

Sasa Waheshimiwa Wabunge wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anaahirisha alipokuwa anataja tarehe ya kukutana tena kwa mara nyingine ilitajwa tarehe 14 Novemba, lakini nimepata rekebisho hapa kwamba itakuwa mapema zaidi kidogo, tarehe 6 Novemba, ni sawa Katibu? Ni tarehe 6 Novemba, tunaomba radhi au twende 14?

WABUNGE FULANI: Hapania.

SPIKA: Turudi 6 eeh?

WABUNGE FULANI: Ndiyo.

SPIKA: Kwa nini mnataka tuharakishe? Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge ni tarehe 6 Novemba, tuweke ratiba/*diary* zetu vizuri.

Basi baada ya hayo naomba sasa tusimame, kwa maana hiyo, sasa naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi tarehe 6 Novemba, 2018, kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyosema.

*(Saa 5.50 Asubuhi Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumanne,
Tarehe 6 Septemba, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*